

**JAMES TENA DIMBANI FEBRUARI**

UKURASA 22


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Alhamisi Desemba 14, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581524

0745 700710 LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com


# CWT ndani kwaumana



• **Maadhimisho** yaahirishwa, Ndalichako ataka Rais asihusishwe... *Endelea ukurasa 2*



Basi lenye namba za usajili T 608 DMP mali ya kampuni ya BATICO lililokuwa linatoka Mwasubuya wilayani Bariadi, Simiyu kwenda Mwanza, likiwa limetumbukia katika Mto Simiyu na kusababisha kifo cha mtu mmoja na kujeruhi wengine 25 jana. **PICHA: VITUS AUDAX**

UKURASA WA 3

**Muhimbili** yazindua mtambo matibabu kwa mgandamizo hewa ya oksijeni



UKURASA WA 4

**Korti** yaamuru bosi wa TUICO kuwasilisha hoja za rufani yake



UKURASA WA 19

**UN** yataka usuluhishi Ukanda Gaza

## Papa Francis ataka akifa asizikwe Vatican

UKURASA 19



## Wanaume waongoza vifo ajali barabarani

UKURASA 2

**MICHEZO** **BONITO, MANGOLO WAKARIBIA YANGA SC** UK.24

**KATUNI** UK.6



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuff Masauni (katikati), akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuhusu taarifa ya ajali, vifo na majeruhi kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, mwaka huu. Kulia ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Maduhu Kazi. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# CWT ndani kwaumana

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KIMEUMANA. Hiyo ndiyo hali inavyoonekana ndani ya Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kutokana na sarakasi zinazoendelea ndani ya chama hicho.

Hali inaonekana si shwari na sasa chama hicho kimeahirisha maadhimisho ya sherehe za kutimiza miaka 30, yaliyopangwa kufanyika keshokutwa, jijini Mwanza kutokana na sababu mbalimbali.

Miongoni mwa sababu hizo ni aliyekuwa akitarajiwa kuwa mgeni rasmi, Rais Samia Suluhu Hassan, kuueleza uongozi wa chama hicho kuwa hatoshiriki kutokana na dharura ya kikazi.

Wakati sababu hiyo ikitolewa kuwa mojawapo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amesema Rais Samia asihusishwe na suala hilo.

Rais wa CWT, Leah Ulaya, alibainisha hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuahirishwa kwa sherehe za miaka 30 ya CWT.

"Maadhimisho ya miaka 30 ya Chama cha Walimu Tanzania kwa hali ninayoiona nikiwa kama msemaji mkuu wa chama, hatutaweza kuendelea nayo kwa sasa kwa kuwa lazima tuangalie tija.

"Tulitarajia kuwa na mgeni rasmi Rais Samia Suluhu Hassan katika sherehe hizo na alisharidhia kushiriki. Akiwa kiongozi mkubwa angekuwa mtu sahihi wa kuja na kusikiliza changamoto zetu na kuzitolea majibu. Baada ya muda tulipata barua kuwa amepata dharura ya kikazi. Hivyo hatashiriki," alisema.

Pia, alisema lengo la kutaka Rais kuwa mgeni rasmi ni kumpata mtu ambaye atasikiliza kero za walimu na kuzifanyia kazi.

"Lengo la kuwa naye ni kusikiliza changamoto zetu na kuzifanyia kazi na kama atakuwa hana nafasi basi kwa ridhaa yake atupangie mwakilishi mwingine ambaye ataona anafaa kuja kusikiliza kundi hili kubwa la walimu," alisema.

Pia alisema sababu nyingine ambayo imewafanya kuahirisha sherehe hizo ni

Uwanja wa CCM Kirumba, jijini Mwanza, ambao waliuomba na kupatiwa kwa ajili ya tukio hilo wameelezwa siku hiyo utakuwa na shughuli nyingine.

"Kutokana na idadi kubwa ya walimu nchini, eneo ambalo lilikuwa linatosheleza idadi yetu ni uwanja wa CCM Kirumba lakini tumepewa taarifa kuwa tarehe ya tukio letu utakuwa unatumika kwa shughuli nyingine.

"Tunashukuru uongozi wa CCM kwa kutupatia taarifa mapema maana yake kama wangechelewa na walimu kuanza kuingia pale Mwanza ingekuwa shida kwao. Kwa hiyo kutokana na hali hiyo, tunaomba tusogeze mbele hadi hapo tutakapopanga tena," alisema Ulaya.

Kadhalika, alisema sababu nyingine ni maneno ambayo yamekuwa yakisambaa kwenye mitandao ya kijamii kueleza kuwa kutakuwepo na uvunjifu wa amani kama maadhimisho hayo yatafanyika.

"Kuwapo kwa dalili za uvunjifu wa amani pia ni sababu lazima turudi nyuma kuona nini shida ili kujiridhisha na kupanga siku ya maadhimisho ambayo yatakuwa na tija hata fedha zitakazo tumika kuleta tija kwa walimu na siyo kufanya ili mradi tuwe tumefanya," alisisitiza.

Hata hivyo, alisema kutokana na hali hiyo anawaomba walimu ambao walikuwa wamejipanga kuanza safari ya kwenda Mwanza kwa ajili ya maadhimisho ya sherehe hizo za miaka 30 ya CWT, kuendelea na majukumu yao mengine hadi hapo watakapo taarifiwa.

Desemba Mosi, mwaka huu, Mwalimu Anatory Kazoba, alimwandikia barua Katibu Mkuu wa CWT, Japhet Maganga, akitaka kusitishwa maadhimisho ya sherehe zilizopangwa kufanyika jijini Mwanza.

Kwa muda mrefu chama hicho kimekuwa na mvutano baina ya wanachama na uongozi, huku baadhi ya wanachama wakilalamika uendeshaji wa mambo hasa matumizi.

**RAIS ASIHUSISHWE**

Waziri Ndalichako jana alikanusha taarifa iliyosambaa mtandaoni ya kuahirishwa kwa maadhimisho ya miaka 30 ya CWT ikimuhusisha Rais Samia kuahirisha kuwa mgeni rasmi katika sherehe hizo.

Akizungumza jijini Dar es Saalam, Prof. Ndalichako aliweka wazi kuwa Septemba 12, mwaka huu, ofisi yake ilipokea mwaliko kutoka CWT ya kuomba Rais Samia kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ambayo yangefanyika Novemba 4 na Rais aliridhia huku akikitaka chama hicho kufanya maadhimisho hayo Novemba 14.

Waziri huyo alisema Novemba 6, 2023 ofisi yake ilipata barua kutoka CWT, ikiomba kusogezwa mbele tarehe ya maadhimisho hayo hadi Desemba 13 na kwamba barua ilijibiwa kuwa Rais atakuwa na majukumu mengine ya kitaifa.

Pro. Ndalichako alisisitiza kuwa hadi sasa hawajapokea taarifa rasmi kutoka CWT inayoonyesha sababu za kuahirishwa kwa maadhimisho hayo, hivyo kutaka kutomhusisha Rais kama chanzo cha kushindwa kuendelea na sherehe hizo.

Hata hivyo, aliweka bayana kuwa Rais Samia anawathamini na anatambua mchango wa walimu na vyama vyote vya wafanyakazi katika ujenzi na kuchagiza maendeleo ya nchi hii.

## Wanaume waongoza vifo ajali za barabarani 2023

**Na Christina Mwakangale**

AJALI 1,641 zimetokea barabarani katika kipindi cha kuanzia Januari Mosi hadi jana, zikisababisha vifo vya watu 1,550, huku wanaume wakiwa 1,189 (asilimia 76.7).

Vilevile, katika ya majeruhi 2,562 wa ajali hizo, wanaume waliojeruhiwa ni 1,721 (asilimia 67) huku wanawake wakiwa 841 (asilimia 33), madereva 1,226 wakifikishwa mahakamani.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alibainisha hayo jana, mkoani Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari baada ya kuhitimisha kikao na wadau wa usalama barabarani.

Kikao hicho kilihusisha Baraza la Usalama Barabarani na wadau mbalimbali, wakiwamo maofisa na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani.

Waziri Masauni alifafanua kuwa takwimu za ajali kwa mwaka huu, zinazoonesha kuwa kati ya ajali 1,641, zimo zilizosababishwa na uharibifu wa vyombo vya moto, akizitaja ni ajali 135.

"Madereva waliofungiwa leseni kwa kipindi hicho ni 2,596 kutokana na makosa mbalimbali," Waziri Masauni alibainisha.

Alipotafutwa na Nipashe jana jioni kuzungumzia ajali hizo, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ramadhani Ng'anzi, alisema zimegawanywa katika makundi matatu.

Aliyataja ni ya ajali zitokanazo na matendo ya binadamu yakijumuishwa uzembe, kutotii Sheria ya Usalama Barabarani, kutojali, mwendokasi, ulevi na kwamba eneo hilo ni chanzo cha ajali kwa asilimia 80 nchini.

SACP Ng'azi anasema kundi la pili ni ubovu wa chombo, akisema si chombo tu kilichombeba abiria na kupata ajali, bali hata kilichomo barabarani kama vile baiskeli, guta na bodaboda vinapokuwa na kasoro.

"Ubovu wa gari unaweza usiwe wa gari au chombo chote cha moto. Kama chombo hakina breki, kinaweza kusababisha ajali kwa chombo kingine na ikatokea athari kubwa kwa sababu ndogo tu," alisema.

Alitaja kundi la tatu ni miundombinu ambayo si rafiki kwa watumiaji; palipo na shimo, hakuna alama za kutoa maelekezo kwa mtumiaji akiwamo dereva aliye mbali.

"Ingawa sababu ya wanaume kufa zaidi, wanasaikolojia watakwambia ni majukumu mengi kwao. Mwanaume utamkuta vitani, barabarani, amekwenda kuwinda, anatafuta kipato," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, alipotafutwa na mwandishi wa habari hizi jana, alisema sekta ya usafirishaji imeajiri zaidi wanaume kuliko wanawake. Ndicho chanzo cha kundi hilo kuathiriwa zaidi na ajali.

"Zamani ilikuwa hivyo kwamba katika udereva mwanamke hawezi kuendesha na katika usafiri wa umma ndiko kulikuwa hakuna au madereva wachache ni wanawake.

"Hivyo, wanaume wataathiriwa zaidi kutokana na madereva wengi ni wao. Shughuli nyingi za kiuchumi wanaume ni wengi na wanasafiri barabarani. Ikitokea ajali wao wataathiriwa zaidi," alisema.

Dk. Anna pia alisema ipo dhana imejengeka kwamba wanawake ni waangalifu zaidi barabarani, wakihofia mengi kama vile wanapopata tatizo, wao ni walezi, familia zitaathirika.

"Sijapata uthibitisho ila wanawake wanakuwa makini zaidi, akihofia kuiacha familia yake, Yaani anakuwa makini zaidi akiwa barabarani na huwezi kukuta mwanamke anaendesha akiwa amepata kilevi, mara chache," alisema Dk. Anna ambaye katika kutekeleza majukumu yake ya ofisini LHRC, anaendeshwa na dereva mwanamke.

# Muhimbili yazindua kituo matibabu mgandamizo hewa njia ya oksijeni

**Na Jenifer Gilla**

HOSPITALI ya Taifa ya Muhimbili imezindua mtambo wa kwanza unaotumia hewa yenye mgandamizo ya oksijeni kutibu zaidi ya magonjwa 10 wenye gharama ya Sh. milioni 250.

Kutokana na kuwapo kwa mtambo huo, Tanzania inakuwa nchi ya kwanza kutumia mtambo unaotoa huduma hiyo katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na ya pili kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara .

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa mtambo huo jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Muhimbili, Prof. Mohamed Janabi, alisema mtambo huo utaleta matumaini mpya kwa wagonjwa waliokuwa wanapata changamoto mbalimbali na kukosa tiba sahihi.

Prof. Janabi alisema wagonjwa wanaohitaji huduma hiyo, wakiwamo watoto wenye usonji, wataingizwa katika mtambo huo unaotumia hewa mgandamizo ya oksijeni kwa asilimia 100 na kupatiwa matibabu.

"Inawezekana baadhi yao walipoteza uhai au kuishia kupata ulemavu wa maisha ikiwamo kukatwa miguu na wengine kupata makovu yatokanayo na vidonda. Uzinduzi wa kituo hiki utaleta matumaini mapya na faraja kwa wagonjwa na wananchi ambao walikuwa wanapata changamoto za matibabu mbalimbali ambayo kwa namna moja au nyingine walikosa majibu," alisema Prof. Janabi

Alisema uwapo wa mtambo huo unadhihirisha azma ya serikali ya kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi nchini na kusogeza huduma hizo karibu na wananchi.

Prof. janabi alitaja wagonjwa watakaotibiwa na mtambo huo kuwa ni wenye vidonda sugu ambavyo matibabu mengine yameshindikana kama wagonjwa wa sukari, walioathirika na moshi baada ya kuungua na moto, waliopata changamoto za upungufu wa oksijeni mwilini na watoto wenye usonji.

Wengine ni wenye upungufu mkubwa wa damu ambao kwa njia moja au nyingine hawawezi kuongezewa damu, waliopata ajali na kupata majeraha mwilini yasiyopona, wenye maambukizi kwenye mifupa isiyopona na waliofanyiwa upasuaji na kupandikiziwa sehemu ya miili yao na Wenye changamoto ya oksijeni kwenye mishipa ya damu.

Prof. Janabi alitaja pia wagonjwa waliopata mionzi na kusababisha sehemu zilizopata tiba mionzi kuathirika ikiwemo wenye saratani za koo, njia ya chakula na wale wenye tezi dume, wenye changamoto ya kusikia ambao vipimo vimeshindwa kuonyesha tatizo na wenye tatizo la usaha kwenye ubongo.

# Daktari bingwa wa MOI atoa ushahidi kesi kupigwa nyundo

**Na Grace Gurisha**

DAKTARI Bingwa wa Mifupa kutoka Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), Joel Mwinza (44), ameeleza mahakamani namna alivyomtibu Deogratus Minja aliyedaiwa kushambuliwa kwa nyundo na mfanyakazi wa benki, Ibrahim Masahi.

Dk. Mwinza alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Amos Rweikiza wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni, Dar es Salaam wakati akitoa ushahidi wake dhidi ya Masahi anayetuhumiwa kumshambulia kwa nyundo Minja Januari 11 mwaka huu huko Mbezi Msakuzi, Dar es Salaam.

Alidai kuwa Januari 24 mwaka huu, alimpokea mgonjwa anayeitwa Deogratus ambaye alipelekwa kwake na daktari kutoka Kitengo cha Dharula cha MOI akiwa na historia ya kujeruhiwa na jirani yake. Alipelekwa kwake ili amtibu mifupa.

"Alikuwa na majeraha kichwani, mgongoni, mkononi, alikuwa amechanika kichwani, ameshonwa nyuzi na pia bega la kulia lilikuwa na maumivu, nilimfanyia vipimo, X-ray ilionesha amevunjika bega na CT Scan ilionesha ameumia kwenye ubongo," alidai Dk. Mwinza.

Alidai kuwa baada ya vipimo, akaanza kumpatia matibabu kwa kumwandikia dawa na katika tatizo la bega alimpa kifaa tiba ambacho alikitumia kwa muda wa wiki sita na kwa upande wa majeraha yaliyoshonwa yalisafishwa na kutolewa nyuzi.

" Mgongwa alinipa fomu ya polisi PF3 nikaijaza, nikampangia siku. Baada ya wiki mbili arudi tena MOI kwa ajili ya uchunguzi. Sikumbuki tarehe, lakini ninakumbuka niliitwa na uongozi ili nitoe ushirikiano kwa polisi kuhusiana na mlolongo wa matibabu niliyompa Deogratus," alidai.

Dk. Mwinza aliendelea kudai kuwa daktari mwenzake alimpokea Minja Januari 12 mwaka huu. Alikuwa amepewa rufani kutoka Hospitali ya Bochi. Akaiomba mahakama ipokee fomu hiyo kama kielelezo katika kesi hiyo. Fomu ilipokewa kwa kuwa Wakili wa Utetezi, Nestory Wandiba hakuwa na pingamizi.

Katika ushahidi wake, Minja alidai kuwa tarehe hiyo, saa 2:30 usiku, alikuwa anapita nje ya geti la jirani yake Masahi. Alimkuta kijana wa jirani huyo, baada ya kumwona, alizungumza kwa kilugha kwa sauti kubwa. Hakuelewa walichozungumza. Baadaye jirani yake huyo alimpiga kwa nyundo kichwani.


**The Guardian Limited**

**VACANCY**

**Freelancer Sales Executive**

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, Arusha and Zanzibar**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 28th December, 2023.**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA NISHATI**
**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

ewura

**TAARIFA KWA UMMA**

**(Imetolewa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni ya 20 (4) ya Kanuni za Mafuta Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Rejareja na Matumizi Binafsi), Gazeti la Serikali Toleo Na. 150 la 2022)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo cha mafuta kama ifuatavyo: -

**Jina la awali la kituo** : Thunderbolt Group Limited -Babati
**Nambari ya Leseni** : PRL-2023-132
**Mahali Kituo kilipo** : Kiwanja Na. 117, Eneo la Ngarenaro, Wilaya ya Babati, Mkoa wa Manyara

**Jina linalopendekezwa** : Dash Petroleum Limited – Babati
**Mmiliki wa awali** : Thunderbolt Group Limited
**Mmiliki mpya** : Dash Petroleum Limited

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne tokea tarehe ya tangazo hili.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA

# Korti yamwamuru bosi TUICO kuwasilisha hoja za rufani yake

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imemtaka Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara na Taasisi za Fedha na Huduma na Ushauri (TUICO), Boniface Nkakatisi, kuwasilisha hoja za rufani yake kupinga hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Wilaya Ilala ya kutupilia ombi lake la kutaka alipwe Sh. milioni 200 kwa madai ya kudhalilishwa na mwanachama ifikapo Desemba 28, mwaka huu.

Nkakatisi alikimbilia mahakamani kumshtaki aliyekuwa Mwenyekiti wa TUICO wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Tawi la Mikocheni Kinondoni, Mambo Mkufu, kwa madai kuwa aliandika barua ya kumkashfu na aliandaa mkutano wa waandishi wa habari na kumdhalilisha.

Kutokana na madai hayo, Nkakatisi aliiomba mahakama imwamuru Mkufu kumlipa fidia ya Sh. milioni 200 kwa udhalilishaji aliyomfanyia, lakini Agosti 3, 2023 mahakama hiyo katika hukumu yake ilitupilia mbali madai hayo.

Katibu mkuu huyo hakukubaliana na hukumu hiyo ndipo alikata rufani Mahakama Kuu kupinga uamuzi huo. Rufani hiyo iliitwa jana mbele Naibu Msajili, Sundi Fimbo, kwa ajili ya kuanza kusikilizwa.

Wakili wa Nkakatisi, Mathew Kabunga, alidai kuwa rufani hiyo iliitwa kwa ajili ya kusikilizwa, lakini wanaomba hoja zao waziwasilishe kwa njia ya maandishi. Fimbo aliimwuliza Mkufu hukusiana na suala hilo akadai kwamba hana pingamizi.

Kutokana na kutokuwapo na pingamizi, Fimbo aliwataka waziwasilishe hoja hizo Desemba 28,2023 na mjibu rufani (Mkufu) awasilishe majibu ya hoja hizo kwa njia ya maandishi Januari 11, 2024 na kama kutakuwa na nyongeza ya hoja yoyote, mkata rufani atawasilisha mahakamani hapo Januari 18,2024.

Akitoa uamuzi huo katika kesi hiyo ya madai ya kashfa namba 79 ya mwaka 2021, Hakimu Mkazi Mwandamizi Rehema Lyana alisema mlalamikaji hakuleta ushahidi wowote wa kuthibitisha madai hayo.

Pia alisema hakuna ushahidi unaoonyesha au kuthibitisha mlalamikaji alivyoteseka ili kuiwezesha mahakama kumpatia hasara ya jumla kama ilivyoombwa.

"Zaidi ya hayo, ili udhalilishaji usimame, maneno yanayolalamikiwa lazima yafafanuliwe kwa uthabiti na lazima yawe ndani ya maana yake yawe ya kukashifiwa," alisema Hakimu Lyana.

Hakimu Lyana alisema kupitia barua hiyo hakuna mahali inayoonyesha kuwa Mkufu alimkashifu mlalamikaji kwenye vyombo vya habari, kwenye ofisi, vyombo vya usalama na magazeti.

Katika hati ya madai, Nkakatisi anadai kuwa Mkufu ambaye ni mwanachama wa TUICO, kutokana na ajira yake TANESCO, Julai 19, 2021, kwa nia ovu na bila kuwa na sababu halali alisababisha kuchapishwa kwa maneno yenye kashfa dhidi yake.

Nkakatis ambaye anawakilishwa na Wakili Mathew Kabunga pia anadai kuwa Mkufu alisababisha kusambazwa kwa barua yake yenye maneno ya kashfa dhidi yake ya Julai 19, 2021.

Alidai kuwa katika barua hiyo ambayo Mkufu alimwandikia yeye kama Katibu Mkuu wa Tuico, kumshambulia yeye binafsi kwa jina lake kwa kusudi la kumharibia hadhi yake kutokana na kile anachokiita maelezo ya uongo.



Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji Jacobs Mwambegele (wa pili kulia), akiongoza kikao cha pamoja kati ya Tume ya Uchaguzi Tanzania na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) kilichokutana jana Mjini Zanzibar. Wengine pichani ni Mwenyekiti ZEC, Jaji George Kazi (wa pili kushoto), Makamu Mwenyekiti wa ZEC, Jaji Aziza Iddi Suwedi na Makamu Mwenyekiti wa NEC, Jaji wa Rufaa (Mst). Mbarouk Salim Mbarouk. **PICHA: NEC**

# Wanane wafariki dunia kwa ajali ya maji

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

WATU wanane wakiwamo watoto sita wenye umri chini ya miaka saba, wamefariki dunia kwa ajali ya maji katika matukio tofauti yaliyotokea ndani ya siku saba Iramba, mkoani Singida.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, alitoa takwimu hizo juzi wakati akitoa salamu za rambirambi kwenye msiba wa mtoto Anson Jackson mwenye umri wa miezi saba.

Mtoto huyo alifariki dunia baada ya kutumbukia kwenye kisima cha maji nyumbani kwao katika tukio lililotokea mjini Kiomboi.

"Tangu tumeanza mwezi Desemba, mwaka huu, leo (juzi) ni siku 12 ambapo ndani ya wiki moja ya mwezi huu tumepokea taarifa za vifo vya watu wanane vinavyotokana na ajali ya maji," alisema.

Mwenda alisema watu hao wamepatwa na maafa hayo kwa kutumbukia kwenye visima na mashimo yaliyojaa maji kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema kati ya waliofariki kijana mmoja wa Kijiji cha Ndurumo, Kata ya Kidaru mwenye umri wa kati ya miaka 18 na 21, alifariki dunia kwa kusombwa na maji wakati alitaka kuvuka maji katika Mto Ndurumo alipokuwa akitoka kwenye shughuli za kutafuta riziki.

Mwenda alisema tukio lingine lililotokea kijiji cha Ndago ambapo wanawake watatu, mwanamume na watoto wanne wenye umri wa miaka mitatu, minne, mitano na saba, walifariki dunia kwa kusombwa na maji wakati wakijaribu kuvuka.

Kutokana na matukio hayo, mkuu huyo wa wilaya awewataka wananchi kuchukua tahadhari kwa kufunika visima kwa mabati kwa kuwa bado kuna dalili za mvua nyingi kuendelea kunyesha.

"Ili kupunguza vifo vinavyotokana na maji tuhakikishe hatutupi taka kwenye mifereji ya maji hali itakayosababisha izibe na maji kujaa kwenye nyumba za watu na kuleta magonjwa ya mlipuko," alisema.

# Mchengerwa awatangazia 'kiama' vigogo halmashauri

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohamed Mchengerwa amewatangazia 'kiama' viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wasiokamilisha miradi ya afya na elimu iliyopata fedha ifikapo Desemba 31, mwaka huu.

Amesema hatosita kuwasemea kwa Rais watenguliwe kwenye nafasi zao kwa kushindwa kukamilisha miradi hiyo kwa wakati huku wananchi wakisubiri miundombinu hiyo.

Mchengerwa (chini) alitoa angalizo hilo jana wakati wa hafla ya uwasilishaji wa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 - 2025 katika Jimbo la Vunjo kwa kipindi cha mwaka 2022/23.

Alisema serikali imetoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hususani ya elimu na afya. Imeshatekeleza jukumu lake. Sasa kazi ni kwa viongozi kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kabla ya Desemba 31 mwaka huu.

"Watanzania wanalipa kodi. Fedha zinakuja kwenye halmashauri zinatumika vibaya; ubadhirifu, uzembe! Mimi kama waziri, lazima nimsaidie Rais kwenye hili.

"Kiongozi ambaye hatakamilisha miradi hiyo mpaka kipindi hicho, atachukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kuondolewa kwenye nafasi hiyo ili tuwape wengine wenye uwezo wa kufanya kazi.

"Nafasi hizi tumepewa kwa kuaminiwa sana na inabidi tufanye kazi kwa kujitoa ili kuwahudumia wananchi.

"Sasa wewe unapewa fedha za miradi unakaa nazo na miradi haijakamilika huku wananchi wanashindwa kupata huduma kwa sababu mtu mmoja tu ameshindwa kutekeleza majukumu yake. Huyu hatuwezi kumfumbia macho, lazima achukuliwe hatua," alionya.

Waziri Mchengerwa aliagiza, "kila mmoja ajitafakari anatekeleza majukumu yake ipasavyo? Ukiona huwezi kwenda na kasi yetu, ni bora ukae pembeni kwa kuwa malengo yetu ni kuhakikisha wananchi wetu wanapata huduma bora kupitia utendaji kazi wetu."



Mchengerwa yuko katika ziara ya kikazi mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Singida, Kagera, Geita na Mwanza.

TANGAZO

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# EXCITING CAREER OPPORTUNITY

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the strategic business needs which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line of its mission of provision of reliable, safe, and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the following positions: -

**1. POSITION: SALES AND MARKETING OFFICER II –TLO (9 POSTS)**

**1.2: MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS:**

- Must have Bachelor Degree in any field.
- Must have one of the following certificate; Air Transport Management, Air Ticketing, or equivalent qualifications from any recognized Aviation institution.
- Possession certificate of IATA or UFTAA will be added advantage.
- Must be computer literate.

**1.3: DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Supervise and ensure efficient and effective check in and boarding of passengers in compliance with carriers' policy/ procedures and customer expectations.
ii. Supervise baggage handling and prepare weekly baggage handling report. Liaise with the GHA to ensure lost baggage is communicated, traced and delivered to affected passengers.
iii. Ensure customers are well handled at all times and especially during flight irregularities and are provided with required assistance.
iv. Ensure conformity with all regulatory requirements, organization standards and local procedure as well as requirements of customer airlines.
v. Effective communication internally and externally to enable effective planning control and reporting
vi. Ensure a safe and secure working environment in compliance with relevant legislative/ industry requirements.
vii. Audit, review and report on service delivery to monitor compliance on SLA's availed to GHA.
viii. Administrative processes to ensure integrity and accuracy manual and computerized data processing.
ix. Strict control of excess baggage collection and remittance.
x. Record all flight movements as per company requirement.
xi. Any other duties as may be assigned by your supervisor.

**2. POSITION: GROUND SERVICE EQUIPMENT OPERATOR II- (1 POST)**

**2.1: Direct Entry Qualifications**

- Must be a holder of Form IV Certificate
- Must have Class "E" or "F" or "G" current Driving License and Professional Ground Support Equipment Level I or its equivalent qualification from recognized institutions.
- Must hold an Airport driving permit from a recognized airport.
- Any experience in Ramp operation would be considered an advantage.

**2.2: DUTIES AND RESPONSIBILITIES:**

i. Operate equipment as per company/ airline procedure.
ii. Repair and service tow tractors, baggage carts, buses, trucks and service vans
iii. Provide on-site GSE support when required
iv. Maintains heavy equipment that includes hydraulic, pneumatic and electrical machinery
v. Inspects ground support vehicles and equipment to determine whether repairs are needed.
vi. Troubleshoots issues or problems with vehicles and machinery as necessary to make repairs
vii. Schedules periodic maintenance for ground support vehicles and equipment
viii. Maintains a clean and safe repair shop
ix. Tracks inventory of parts and tools needed for repairs and maintenance
x. Maintains repair log for vehicles and equipment
xi. Provide training to GSE operators as required by ATCL operational requirements
xii. Report any incident or damage immediately as per company procedure.
xiii. Perform any other official duties as may be assigned by your supervisor.

**3 POSITION: AVIATION SECURITY ASSISTANT II (2 POSTS)**

**3.1: MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE**

- Must be a holder of an Advanced Secondary School Certificate or a Diploma preferably in Law plus training/certification on military/militia or its equivalent qualifications from recognized institution.
- Must have Aviation Security Screener Training
- Training in Cargo and Mail Security, Airport Security or Security Quality Control will be an added advantage.

**3.2: DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Ensure proper access control of staff, authorized persons and vehicles to aircrafts
ii. Conduct aircraft security searches and checks as appropriate
iii. Ensure that security personnel from outsourced security service providers are appropriately deployed and supervised to ensure for security of aircrafts, passengers, baggage, cargo and mail.
iv. Ensure Revenue Integrity.
v. Report and record all incidents in the OB for management follow up
vi. Brief and debrief outsourced security on security matters to ensure they understand and implement the instructions.
vii. Ensure safe and secure handling and carriage of firearms in compliance with company security program
viii. Prepare daily shift security operations report to ensure that there is proper follow up and action on any issues arising in course of duty.
ix. Ensure safe custody and accountability of Lost and Found property until reclaimed by the rightful owner or otherwise disposed of according to company policy.
x. Act as duty shift in-charge
xi. Perform any other official duty as may be assigned by your Supervisor

**4 POSITION: PROCUREMENT OFFICER II (2 POSTS)**

**4.1: MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS:**

- Must be holder of Bachelor Degree in one of the following fields; Procurement and Supplies Management, Material Management, Logistics Management or equivalent qualifications from a recognized institution.
- Must be registered by PSPTB as Graduate Procurement and Supplies Professional.

**4.2: DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. To prepare bid documents and Tender advertisements
ii. To prepare contract documents or purchases orders to approved bidders
iii. To seek approval to purchase the identified requirements
iv. To participate in preparation of Annual Procurement Plan (APP)
v. To participate in preparation of monthly, quarterly and annual procurement reports
vi. To receive, verifying, and submitting Invoice of delivered goods or completed service for payment
vii. Participate in preparation for stock taking
viii. Liaise with suppliers for timely delivery of the goods
ix. To maintain store records
x. To receive and Issue goods to user department, processing stores requisitions, order expedition, inventory and stock replenishment
xi. To perform any other related duties as may be assigned by the supervisor.

**5 POSITION: PROCUREMENT ASSISTANT II- (6 POSTS)**

**5.1: MINIMUN ENTRY QUALIFICATION**

- Holder of Certificate in one of the following fields; Procurement and Supplies Management, Material Management, Logistics Management or equivalent qualifications from a recognized institution.
- Must be registered by PSPTB as Procurement and Supplies Technician or Procurement and Supplies Full Technician.

**5.2: DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

i. Carry out a range of maintenance support, distribution, warehousing, and storage tasks. distributing and/or delivering materials, data entry, inventory control, retrieving parts, tools, or units, and stocking.
ii. Responsible for ensuring that the cycle count program is accurately implemented, distribute and convey paperwork, materials, and parts to and from the storage or work site to designated areas
iii. To replenish inventories to appropriate levels
iv. Accurate Data entering for all parts into the area, as well as material movement transactions (transfers, issues, returns and cycle counts).
v. Ensure proper marking of raw material and shelf life sensitive parts/materials according to company procedures.
vi. Execute the requirements of the reference manual (including the proper use of forms) and Quality Control Manual. Handle tagging and quarantine procedures.
vii. Deal with the processes and policies for repair stations and customs.
viii. Prepare, review, and submit the monthly activities as required by the Line Manager.
ix. Report incidents/accident occurrences following company procedures.
x. Adhere to the company safety, health, and environmental policy.
xi. Perform any other duties to be assigned by the supervisor

**6. TERMS AND CONDITIONS:**

- Ten (10) years contract with attractive remuneration and fringe benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.
- Candidates should be willing to work up country apart from Dar es Salaam if required to.

**7. MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:**

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the application attached with the following:

i. A curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school, birth certificates), other relevant certificates, Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)
iii. Two recent passport size photographs
iv. Name and address of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

**8. CLOSING DATES:**

Applicants should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement.

**MANAGING DIRECTOR & CEO,**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM.**
**Date: 14th December, 2023.**

***ATCL is an equal opportunity employer. Women are encouraged to apply. Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences.***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Suala hili la bidhaa bandia litafutiwe jawabu mwafaka

**SHIRIKISHO** la Viwanda Tanzania (CTI) juzi lilifanya mkutano wake mkuu wa mwaka ambao ulijadili na kufanya tathmini ya mambo mbalimbali kuhusiana na shughuli zake. Mkutano huo ulikuwa na umuhimu wa kipekee kutokana na ukweli kwamba viwanda ni mhimili katika maendeleo ya uchumi hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchumi wa kati.

Pamoja na kupata fursa ya kujadiliana mambo hayo, moja ya mambo yaliyojitokeza ni kushamiri kwa bidhaa bandia na feki katika masoko nchini. Mkurugenzi wa Kudhibiti Bidhaa Bandia kutoka Tume ya Ushindani (FCC), Khadija Ngasongwa, alibainisha hilo wakati akitoa mada kwenye mkutano huo.

Mkurugenzi huyo kutoka mamlaka ambayo pamoja na mambo mengine inahusika na udhibiti wa bidhaa bandia na zisizo na viwango ili kuwa na ushindani halali katika soko, alibainisha kuwa hivi sasa bidhaa feki zikiwamo vipuri vya magari, pikipiki na vifaa vya umeme, vimezagaa katika masoko nchini. Katika mada yake hiyo, Ngasongwa alisema licha ya jitihada zinazofanywa na serikali katika kudhibiti uingizaji wa bidhaa zisizofaa kwa matumizi, wanaoingiza wamekuwa wakibadilisha mbinu mara kwa mara ili kukwepa mkono wa serikali. Alikiri kwamba bidhaa za aina hiyo zimeongezeka sokoni kwa sababu mahitaji ya vipuri na vifaa vya umeme.

Mbali na kuwapo kwa bidhaa hizo ambazo zinafifisha ushindani wa kibiashara dhidi ya bidhaa halali zikiwamo zinazotengenezwa nchini, alisema bidhaa hizo bandia na hafifu zimekuwa zikisababisha anguko la bidhaa halisi sokoni kutokana na kuuzwa kwa bei ya chini hali ambayo imekuwa ikiwavutia wateja wengi.

Pamoja na FCC kukiri kuenea kwa bidhaa hizo na kuharibu ushindani halali, baadhi ya wananchi walihojiwa katika maeneo mbalimbali mkoani Dar es Salaam na kukiri kuwa hali hiyo iko katika soko. Walibainisha kuwa wafikia madukani kwa ajili ya bidhaa hizo, anaelezwa kinagaubaga kuwa bidhaa za halali zinauzwa bei juu huku zile za viwango dunia zikiuzwa kwa bei ndogo. Kutokana na hali ya uchumi miongoni mwa wananchi. wanaamua kuchagua zile ambazo ni za kiwango cha chini.

Kwa ujumla, kauli hiyo kutoka FCC imeshtua jamii na kuonyesha kuwa kuna hatari ya wananchi wengi kupata hasara kutokana na kutumia bidhaa hafifu au bandia na matokeo yake kupata hasara kwa kununua bidhaa husika ndani ya muda mfupi kisha kutumika na kurejea kununua tena.

Hata hivyo, taarifa hiyo imeibua maswali kadhaa kwa FCC na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), taasisi ambazo zimepewa dhamana ya kuhakikisha hakuna bidhaa zinazoingia sokoni bila kuhakikiwa na kuwa na nembo zao. Miongoni mwa maswali ni je, hakuna ukaguzi unaofanyika katika nchi ambazo bidhaa hizo zinazalishwa? Bidhaa zinaingizwaje nchini bila kukaguliwa? TBS inafanya nini mpaka bidhaa hizo zinaingia sokoni?


Kwa mtazamo yakinifu, TFF imeonyesha udhaifu mkubwa kukiri kuwapo kwa bidhaa hizo katika soko bila kueleza ni hatua gani imechukua ikiwamo kuziteketeza. Katika mada ya mkurugenzi wake, imetoa wito kwa wananchi kuwa waangalifu na bidhaa hizo ili kukwepa kupata hasara badala ya kuchukua hatua kwa mamlaka iliyopewa ya kudhibiti, kukamata na kuteketeza bidhaa hizo.

Ni wakati sasa wa taasisi zilizopewa dhamana kuchukulia maswali kama uingizwaji wa bidhaa bandia au hafifu kwa uzito unaostahili badala ya kuwa sehemu ya kulalamika. Kama serikali inalalamika, wafanyabiashara wanalalamika na wananchi nao wanalalamika, nani mwenye nafasi ya kutoa ufumbuzi juu ya jambo husika? Ni vyema kila mtu akawajibika kwa nafasi yake ili kuyapatia majawabu matatizo yanayoikumba jamii.

Kwa upande wa suala hili la vifaa bandia, ni vyema mamlaka husika zikachukua hatua kudhibiti uingiaji holela ili kuwanusuru wananchi dhidi ya hasara watakazozipata.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Safari ya Nyerere kuusuka uchumi, kuhamia zama uchumi wa viwanda

Na Sabato Kasika

**DESEMBA** 9 Tanzania imehitimisha miaka 62 ya uhuru uliopatikana mwaka 1961, baada ya kuwa chini ya ukoloni uliosababisha Watanganyika kukosa uhuru wa kujiamulia mambo yao wenyewe.

Miaka 62 ya uhuru si haba, kwani kipindi hicho chote wananchi wameendelea kudumisha umoja, mshikamano na amani, huku baadhi ya nchi zimekumbana na mitafaruku mbalimbali.

Nimegusia kidogo, lakini lengo langu ni kutaka kujadili, jitihada za Rais wa kwanza Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alizofanya kwenye sekta ya viwanda ili kuinua uchumi wa nchi.

Wakati nchi inapata uhuru mwaka huo, historia inaonyesha kuwa sekta ya viwanda ilikuwa changa, kwa kuwa kulikuwa na viwanda vichache ambavyo vilikuwa vikichangia asilimia 3.5 ya Pato la Taifa (GDP) na kuajiri asilimia 9 ya ajira zote.

Baada ya kushika uongozi, Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliamua kuweka mkakati wa kuendeleza viwanda ikiwa ni sehemu ya mpango wa kwanza wa miaka mitano mwaka 1964.

Historia inaonyesha kuwa mpango huo uliotoa kipaumbele kwa sekta ya kilimo, kwa ajili kuvutia wawekezaji wa ndani kuanzisha viwanda vitakavyozalisha bidhaa zilizokuwa zinaagizwa kutoka nje ya nchi.

Mara tu baada ya uzinduzi wa Azimio la Arusha mwaka 1967, serikali ilibadili mkakati wa maendeleo ya viwanda uliokuwa unalenga sera ya Ujamaa na Kujitegemea.

Azimio hilo lilijikita katika misingi miwili; kuhakikisha mkakati haulengi katika uwekezaji kwa sekta binafsi na kutaifisha viwanda na mashirika yote yaliyokuwa yanamilikiwa na sekta binafsi.

Kimsingi, Tanzania ni miongoni mwa nchi za Afrika iliobarikiwa kwa kuwa na rasilimali mbalimbali, yakiwamo madini, mbunga za wanyama, misiti, milima na mabonde, maziwa, mito na ardhi yenye rutuba.

Vilevile, ardhi hiyo inaruhusu kuwapo kwa kilimo cha mazao mbalimbali ya chakula na biashara ambayo yanaweza kusaidia katika shughuli za uzalishaji kwenye viwanda.

Kutokana na umuhimu wa rasilimali hizo, alianzisha viwanda vingi ili kujenga taifa imara linalojitegemea kiuchumi, vilijengwa karibu kila mkoa visaidie kuimarisha uchumi kwa kupata malighafi toka kwa wakulima na kutengeneza bidhaa na kuuza soko la ndani na nje ya nchi.

Baadhi ya viwanda hivyo ni kama Urafiki Textile, Mwatex, Mutex, Kiltex, Sungura Textile,Tanganyika Packers na UFI, ambavyo kwa sasa ni kama havipo kabisa kwani havijaishi tena.

Vingine ni Morogoro Cavans kilichotengeneza magunia na marutubai, Moro Shoes, Bora Shoes (viatu), huku vya ngozi vikiwa ni MorogoroTanneries na Mwanza Tanneries.

Pia, kulikuwapo Kibo Match Factory (vibiriti), National, Matsushita na Philips, vilivyotengeneza betri na redio Pamba Enginering cha kuchonga vipuri vya mashine za kuchambua pamba.

Nimejaribu kutaja vichache hivyo, lakini ukweli ni kwamba, nchi ilikuwa na viwanda vingi ambavyo baadaye vilibinafsishwa miaka ya 90 na sasa vingine vimeshindwa kujiendesha na hivyo kufungwa.

Jitihada za Baba wa Taifa, zililenga kupiga hatua katika maendeleo ya taifa kiuchumi na kuwakwamua Watanzania kutokana na umaskini, lakini baada ya uongozi wake mambo yalibadilika.

Mambo yamebadilika kwa sababu baada ya uwekezaji, baadhi ya viwanda vilipoteza mwelekeo na kusababisha ndoto za Baba wa Taifa za kujenga Tanzania ya viwanda zishindwe kutimia.

Nadhani tunaposheherekea miaka 62 ya uhuru, tuangalie ni wapi ambapo tumejikwaa hadi kusababisha viwanda vikongwe kufa na kusababisha kundi kubwa la Watanzania kukosa ajira.

Nakumbuka kuna kiwanda kimoja ambacho Rais wa awamu ya tano, hayati Dk. John Magufuli aliwahi kusema kuna mwekezaji alikichukua badala ya kukiendeleza, anakitumia kufugia mbuzi wake.

Hivyo, ingekuwa ni vyema kama serikali itaangalia viwanda ambavyo walipewa wawekezaji na kushindwa kuviendesha, wapewe wengine ili vifanye kazi na kuwezesha Watanzania kupata ajira.

Si vibaya kuangalia ni wapi ambapo kama nchi tumejikwaa hadi kusababisha viwanda vikongwe kufa na kusababisha kundi kubwa la Watanzania kukosa ajira, ili lifanyiwe kazi.

# Mume aua mke kisha kujiua madai ya wivu wa kimapenzi

Na Christina Haule, MOROGORO

MKAZI wa Kichangani, Manispaa ya Morogoro, Boniface John (26), amemuua mkewe kwa kumchoma visu sehemu mbalimbali za mwili kisha kukimbilia eneo la Bigwa na kujiua kwa kujichoma kisu shingoni na tumboni.

Mauaji hayo yamedaiwa kuwa chanzo chake ni wivu wa kimapenzi baina ya wanandoa hao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi (ACP) lex Mkama, alisema tukio hilo lilitokea juzi usiku katika maeneo ya Mafisa kwa Mambi, wilaya na mkoa wa Morogoro. Alimtaja mwanamke aliyeuawa kuwa ni Devotha Gilbert (20) mkazi wa Mwembesongo, Manispaa ya Morogoro ambaye mwili wake ulitelekezwa katika eneo hilo baada ya kuuawa.

Kamanda Mkama alisema uchunguzi ulipofanyika ulibaini kuwa John ambaye ni mfanyakazi wa machinjioni, baada ya kutekeleza mauaji hayo, aliondoka na pikipiki yake yenye namba MC 711 CQV aina ya OGU, hadi mtaa wa Kindimbwa, Kata ya Bigwa na kujiua kwa kujichoma na kisu shingoni na tumboni.

Mkama alisema uchunguzi wa awali umebaini kuwa chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa kimapenzi na kwamba wawili hao walikuwa na mgogoro wa kifamilia takribani mwezi mmoja uliopita.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio la Mafisa kwa Mambi, Hamadi Kikuu, alieleza kusikitishwa na kitendo cha kinyama alichofanyiwa mwanamke huyo na kusema eneo hilo limekuwa kama la kuuliwa watoto wa kike au machinjio ya watoto wa kike, hivyo kuomba kuwekwe ulinzi wa kutosha.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mafisa kwa Mambi, Hamad Kinyasi, alisema alipokea simu saa 1:00 asubuhi na kufika eneo la tukio na kumkuta mama huyo akiwa ameuawa huku akiwa na jeraha mkono wa kulia linaloashiria kujeruhiwa na kitu chenye ncha.

Alisema pia mbele yake kulikuwa na kisu kilicholoa damu na upande wa mguu wake wa kulia kulikuwa na simu ndogo ndipo alipotoa taarifa polisi kwa mkuu wa upelelezi mkoa ambaye alifika eneo la tukio na kuangalia mwili na kuugeuza mwili huo kwa utambuzi na wananchi waliokuwapo hawamtambua kisha polisi kuondoka nao.



Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Anamringi Macha (kulia), akizungumza na Katibu Mkuu wa Chama Tawala cha Namibia (SWAPO), Sophia Shaningwa, katika ofisi ndogo za makao makuu ya CCM, Mtaa wa Lumumba, jijini Dar Es Salaam juzi. **PICHA: CCM**

# Kiwanda chasaidia waathirika mafuriko

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimewataka Watanzania kulinda miundombinu ya wawekezaji na mali zao kwa kuwa mbali na ajira na kodi kwa serikali, wamekuwa na msaada kwa nchi kunapotokea majanga.

Wito huo ulitolewa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Gilead Teri, wakati akipokea msaada wa gypsum kutoka kiwanda cha KNAUF kilichoko Mkuranga, Pwani.

Teri alipokea msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni 10 kwenye makao makuu ya TIC, Dar es Salaam.

Alisema Watanzania wanapaswa kuwaona wawekezaji kuwa washirika wa maendeleo kwa kuwa licha ya kuchangia kuongeza ajira na kodi kwa serikali wamekuwa msaada kunapotokea majanga mbalimbali.

"Uwekezaji si fedha na ajira tu bali ni msaada kwenye changamoto kama hii ambayo wamepitia wenzetu kwa hiyo nawaomba watanzania waendelee kuwalinda wawekezaji kwasababu watakapopata majanga watawasaidia," alisema.

Teri alisema kiwanda hicho cha uzalishaji bidhaa za ujenzi kutoka Ujerumani kimekuwa cha kwanza kuitafuta TIC kwamba kinataka kutoa msaada kutokana na maafa yaliyowakuta wananchi wa Katesh, Hanang mkoani Manyara.

Alisema kiwanda kimetoa 'gypsum board' zenye uwezo wa kuhifadhi unyevunyevu na utasaidia kwenye ujenzi wa zahanati na shule ambazo zimeathirika kwa mafuriko yaliyotokea.

"Msaada huo una thamani ya Sh. milioni 10 na gari lenye msaada huo limeanza kusafiri kwenda Katesh. Tunaomba wanaokuja kuwekeza nchini wasaidie kwenye majanga kama haya na rafiki wa kweli ni yule anayekufaa wakati wa shida kama hawa KNAUF," alisema Teri.

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa KNAUF, Rose Mero, alisema wameona watoe msaada huo baada ya kuguswa na maafa yaliyotokea kwa watu wa Katesh Mkoa wa Manyara.

"Msaada wetu umelenga kuboresha maeneo ya shule na zahanati zilizoharibiwa na mafuriko haya kwetu sisi tunaona ni muhimu kurudisha kwa jamii kila kunapotokea majanga kama haya," alisema.

## CRDB yatangaza mshindi wa tano wa kampeni yake SimBanking

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imemkabidhi Rehema Lupapa, mkazi wa Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam gari jipya aina ya Toyota Crown baada ya kuibuka mshindi katika awamu ya tano ya kampeni ya 'Benki Ni SimBanking'.

Akieleza namna anavyoitumia huduma za Simbanking, Rehema amesema amekuwa mteja wa Benki ya CRDB kwa miaka mingi na huduma hiyo imekuwa inamrahisishia kufanya miamala mbalimbali kwa urahisi na kwa wakati.

Katika hafla ya kukabidhi zawadi kwa mshindi huyo iliyofanyika katika Tawi la Benki ya CRDB Kijitonyama, Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Benki ya CRDB, Godfrey Rutasingwa, alisema mshindi huyo alipatikana katika droo ya tano ya kampeni hiyo iliyofanyika Desemba 4, mwaka huu jijini Dar es salaam.

Rutasingwa alibainisha kuwa katika kusaidia jitihada za serikali za kuchochea uchumi wa kidijitali nchini, kampeni ya 'Benki Ni SimBanking' imekuwa inahamasisha wateja kufanya miamala kidijitali kupitia SimBanking na kuachana na matumizi ya fedha taslimu.

Akielezea kampeni hiyo, Rutasingwa alisema 'Benki Ni SimBanking' ni kampeni iliyoendeshwa kwa muda wa miezi 10, ambapo kila siku wateja wamekuwa wanajishindia zawadi, huku pia kukiwa na zawadi za mwezi, miezi miwili na zawadi kubwa ya Toyota Vanguard ambayo itatolewa mwishoni wa kampeni.

"Hadi kufikia sasa tayari tumeshatoa zawadi mbalimbali ikiwamo fedha taslimu, simujanja na laptop (kompyuta mpakato) kwa washindi. Hivyo niwasihi wateja na wale wasio wateja waendelee kufanya miamala kupitia SimBanking ili kujijengea mazoea ya kutumia huduma kidijitali," alisema Rutasingwa huku akiwakaribisha wale ambao si wateja wa Benki ya CRDB kufungua akaunti ili waunganishwe na SimBanking.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa gari, mshindi wa shindano hilo, Rehema aliishukuru benki hiyo kwa zawadi hiyo ya gari huku akibainisha siri ya ushindi ni kujenga utamaduni wa kutumia SimBanking kufanya miamala yake yote ya kifedha.

"Ninafurahia sana kufanya miamala kupitia SimBanking iliyoboreshwa, imekuwa rahisi na nafuu sana kutumia.

"Sasa hivi miamala yangu yote ninakamilisha kupitia SimBanking, iwe kufanya malipo kupitia CRDB Lipa Namba, kutuma fedha, kulipia bima, kulipia kodi na kutoa fedha kwa CRDB Wakala/ ATM na katika matawi bila ya kadi," alibainisha Rehema.

# RC aipigia debe Boeing 767-300 ya ATCL

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, amewataka wafanyabiashara nchini kutumia ndege ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) aina ya Boeing 767-300F kutokana na kuwa na uwezo mkubwa wa kubeba bidhaa mbalimbali na kusafiri masafa marefu.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza kwenye kikao cha pamoja cha wadau wa soko la bidhaa za samaki kutoka mkoani Mwanza kilichofanyika Makao Makuu ya ATCL, Dar es Salaam.

Makalla alisema kuwapo kwa ndege hiyo kunarahisishia usafirishaji wa bidhaa za Tanzania hususani minofu ya samaki kwa kusafirishwa moja kwa moja kutoka kanda ya ziwa kwenda kwenye masoko mbalimbali duniani.

Alisema ndege hiyo inawawezesha wafanyabiashara wa minofu ya samaki kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza thamani ya minofu kwa kutumia muda mfupi kufika kwenye soko duniani.

Pia aliwahakikishia wafanyabiashara kuwa wataendelea kushirikisha wadau na wataalam mbalimbali katika kushughulikia changamoto zilizopo ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya uwanja wa ndege wa Mwanza.

Alisema serikali itaboresha jengo la kuhifadhia bidhaa ni kuweka kituo kimoja cha utoaji wa huduma za mamlaka zote za uthibiti, kupitia tozo na taratibu ili kupunguza gharama zisizo za lazima na kuhakikisha bidhaa hizo zinasafirishwa kupitia kiwanja cha ndege cha Mwanza.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Mhandisi Ladislaus Matindi, alisema ATCL pamoja na kufanya biashara inahusika pia na uwezeshaji wa sekta zingine kwa kutoa huduma zinazohitajika ikiwemo kulinda thamani ya bidhaa za watanzania kwa kuzifikisha kwenye soko la dunia zikiwa shindani.

Matindi aliongeza kuwa uwapo wa ndege ya mizigo yenye uwezo wa kubeba mizigo yenye upana mkubwa na uzito wa zaidi tani 50 kwa mara moja ni fursa kwa Watanzania kukuza biashara zao duniani.

Alisema Januari mwakani wanatarajia kupokea ndege nyingine aina Boeing 737 MAX.

Mbali na ndege hiyo itakayokuwa na uwezo wa kubeba abiria 189, alisema mwezi Machi pia ATCL itapokea ndege nyingine kubwa aina ya Dreamliner 787-800 itakayokuwa na uwezo wa kubeba abiria 260.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Deo Ndejembi (kulia), akitoa maelekezo alipotembelea mradi wa ujenzi wa jengo jipya la utawala la Halmashauri ya Muheza jana na kukagua mradi wa Shule ya Msingi Magila, Shule ya Sekondari ya Chatuu na ujenzi wa Shule ya Sekondari Makole. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Waziri aahidi ushirikiano uboreshaji ofisi nyaraka

**Na Lusungu Helela**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete amewahakikishia Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuwa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa iko tayari kushirikiana na Ofisi ya Nyaraka Zanzibar kuhakikisha inaboreshwa kwa maslahi mapana ya pande zote za Muungano.

Kikwete alisema hayo juzi wakati akizungumza na wajumbe wa kamati hiyo mara baada ya kutembelea Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Kanda ya Mashariki jijini Dar es Salaam.

Lengo la ziara hiyo ilikuwa kujifunza na kubadilishana uzoefu wa namna ya kutunza na kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu za taifa.

Naibu Waziri alisema amesema taifa lolote lisilo na kumbukumbu ni taifa lililokosa mwelekeo kwa kuwa halijui limetoka wapi na linakwenda wapi.

Kutokana na umuhimu huo, Kikwete aliiahidi kamati hiyo kuwa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa itatoa ushirikiano wa kutosha ili kuhakikisha kumbukumbu na nyaraka za viongozi wakuu Zanzibar zinatunzwa na kuhifadhiwa kwa maslahi mapana ya taifa.

"Tuko tayari kushirikiana nanyi ili kuhakikisha kumbukumbu na nyaraka za waasisi wa taifa letu zinalindwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya kutusaidia kufanya uamuzi wenye mwelekeo wenye maslahi kwa ajili ya kizazi cha sasa na cha baadaye," alisisitiza.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu Zanzibar, Jamal Kassim Ali, aliitaka Ofisi ya Rais Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka kuunga mkono jitihada mbalimbali ili kuhakikisha Ofisi ya Nyaraka Zanzibar inaboreshwa.

Alisema ushirikiano kati ya Idara ya kumbukumbu na Nyaraka na Ofisi ya nyaraka Zanzibar utasaidia kuratibu na kutunza nyaraka na kumbukumbu za taifa kwa ajili ya kizazi cha sasa na urithi wa vizazi vya baadae.

"Ofisi yetu bado ni changa na hivi karibuni tunatarajia kuanza mchakato wa kutunza kumbukumbu za viongozi wa juu hasa waasisi wa taifa. Tunapoelekea kutimiza miaka 60 ya Mapinduzi, tunatarajia kuwa na namna ya utunzaji wa kumbukumbu za Rais Hayati Abeid Aman Karume, hivyo tunaomba ushirikiano wenu wa hali na mali," alisema.

Pia aliitaka Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka na Ofisi ya nyaraka Zanzibar kuhakikisha zinaweka mikakati ya kuhamasisha na kuuelewesha umma umuhimu wa ofisi hizo ili kuzipa thamani inayoendana na kazi wanazofanya.

Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Machano Othman Said, alisema utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka za taifa ni shughuli muhimu katika maendeleo ya nchi.

Machano aliitaka idara ya kumbukumbu kuendeleza ushirikiano na Ofisi ya Nyaraka Zanzibar katika maeneo ya elimu, vifaa na masuala ya kiutendaji na teknolojia.

## Kamishna amaliza mgogoro wa ardhi polisi na wananchi

**Na Munir Shemweta,** TABORA

KAMISHNA wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Tabora, Hussein Sadiki, amemaliza mgogoro wa muda mrefu kati ya Jeshi la Polisi Kituo cha Nanga na wananchi waliouziwa viwanja ndani ya eneo la jeshi hilo Igunga mkoani hapa.

Sadiki na timu yake walifika katika eneo la mgogoro Desemba 7, mwaka huu, kwa lengo la kukutana na uongozi na wajumbe wa serikali ya kijiji cha Nanga, mkuu wa kituo cha polisi na mtendaji aliyekuwapo wakati wa kubariki uuzwaji maeneo hayo.

Mgogoro wa eneo hilo ulizuka kutokana na wananchi kuuziwa viwanja katika eneo la polisi kwa madai kuwa uuzwaji huo ulibarikiwa kwa pamoja na uongozi wa kijiji na Halmashauri ya Wilaya ya Igunga.

Akizungumza katika kikao cha kutafuta suluhu ya mgogoro huo, Diwani wa Nanga, Robert Jidai, alisema akiwa mwakilishi wa wananchi, alipelekewa hoja kuwa wananchi wameuziwa viwanja kwa kufuata taratibu zote lakini wanazuiwa kufanya maendelezo kwa madai kuwa eneo hilo ni la jeshi la polisi. Alisema hali hiyo ilisababisha yeye kutaka kujua zaidi undani wa suala hilo.

Alisema baada ya kufuatilia kwa undani kwa kuiuliza serikali ya kijiji, alielezwa kuwa uuzwaji viwanja ni mradi wa serikali ya kijiji na ulibuniwa kwa lengo la kuupanga mji sambamba na kupunguza maeneo ya taasisi yaliyo makubwa na mpango huo ulishirikisha taasisi husika likiwamo Jeshi la Polisi.

"Baada ya kuwa tumeapishwa, niliIetewa hoja hii na zaidi ya wananchi 30 wakiwa na hati za viwanja na nilitaka kujua ilikuwaje. Baada ya kuuliza nilielezwa na serikali ya kijiji kuwa huo ulikuwa mradi wa serikali ya kijiji wenye lengo la kupunguza maeneo ya taasisi ambayo ni makubwa," alisema.

Kutokana na maelezo ya uongozi wa kijiji pamoja na kukagua baadhi ya nyaraka za mauziano ya viwanja, Kamishna Sadiki alibaini kwamba kijiji kilikaa kikao kwa madhumuni ya kumega maeneo ya umma na eneo la polisi lilimegwa na kutolewa vipande 51 vya ardhi.

Hata hivyo, alisema upimaji wa vipande hivyo haukupata idhini na hakukuwa na mpango mji ulioidhinishwa na kwamba baadhi ya wajumbe walikuwa wanufaika wa mpango huo.



# Madaktari wapewa mafunzo matibabu ya mionzi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TUME ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) imeandaa mafunzo ya siku tano katika ofisi ya Kanda ya Kaskazini iliyopo jijini Arusha kwa madaktari wanaotoa huduma za mionzi nchini.

Lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha usalama wa eneo la kazi na wagonjwa wanaopatiwa huduma ya mionzi.

Baada ya kufungua mafunzo hayo jana, Mkuu wa Idara ya Huduma za Kiufundi na Kinga za Mionzi TAEC, Yesaya Sungita, alisema lengo la mafunzo hayo ni kutoka elimu kuhusu usalama wa matumizi ya mionzi na kujua namna bora ya kuwakinga wagonjwa dhidi ya mionzi.

Sungita alisema mafunzo hayo pia yanatoa elimu kuhusu mbinu za kujikinga na namna kutumia teknolojia ya nyuklia katika huduma mbalimbali kwenye hali usalama, ili kuhakikisha Watanzania wanalindwa na madhara ya mionzi.

"Kujikinga kunaanzia kwa mtoa huduma, lazima ajue mbinu za kiusalama za kuweza kujikinga na pia amkinge mgonjwa asiathirike na mionzi ya nyuklia na mionzi inayotumika sehemu mbalimbali, ikiwamo kutoa huduma za tiba na uchunguzi wa magonjwa," alisema.

Alisema kuwa baada ya mafunzo hayo, wanatarajia madaktari hao watakaporejea sehemu zao za kazi, usalama utaimarika kwa kuwa wameiva kuhusiana na nyanja hiyo.

Alfred Nzele, daktari kutoka Hospitali ya Wilaya ya Rombo, alisema wameshiriki mafunzo hayo kwa lengo la kupata elimu kuhusu usalama wa matumizi ya mionzi, ili kujua namna bora ya kuwakinga wagonjwa dhidi ya mionzi na wao katika kitengo cha mionzi, hivyo imewasaidia kuongeza mbinu za usalama kwa wagonjwa na wao, wataalamu.

Mtawa Marietha Kurwa kutoka Hospitali ya Singida, alisema mafunzo hayo yatawanufaisha kwa kuwa wamepata ujuzi na maarifa zaidi ya waliyokuwa nayo.

# Mchengerwa aahidi kutatua kero za afya, uhaba watumishi Vunjo

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, ameahidi wananchi wa Vunjo wilayani Moshi, mkoani Kilimanjaro, serikali itamaliza tatizo lao la muda mrefu la kukosekana gari maalum la kubeba wagonjwa kabla ya Desemba 31, mwaka huu.

Pia amemwahidi Mbunge wa Vunjo, Dk. Charles Kimei, serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo kipya cha afya, ambacho mwakilishi huyo wa wananchi bungeni atachagua kijengwe wapi kulingana na uhitaji wa wananchi wake.

Waziri Mchengerwa aliahidi hayo jana alipoalikwa katika mkutano mkuu wa jimbo hilo uliofanyika kwa ajili ya uwasilishaji wa taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025 kwa mwaka 2022/23.

"Katibu Mkuu wa TAMISEMI (Wilson Mahera) upo hapa, mpaka kufikia Desemba 31, mwaka huu uhakikishe umemkabidhi Mbunge (Dk. Kimei) ambulance (gari la wagonjwa).

"Mwenyekiti wenu wa CCM wa Wilaya ya kichama ya Moshi Vijijini (Cyril Mushi) ameeleza kuhusu tatizo la vijiji vingi kukosa watendaji. Tayari Mheshimiwa Rais ameshatoa maelekezo ya kibali cha kuajiri na mimi ninamwagiza DED (Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Moshi), tangaza nafasi 15 za watendaji wa vijiji.

"Kuhusu barabara, ninajua ni changamoto kwa wananchi wetu. Ninamwagiza Mtendaji Mkuu wa TARURA (Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini), Victor Seif, kutangaza zabuni ya kuanza mradi wa ujenzi wa barabara ya Mabogini/Kahe kwa kiwango cha lami, yenye urefu wa kilomita nne.

Mbunge wa Vunjo, Dk. Charles Kimei, wakati anawasilisha taarifa ya utekelezaji ilani ya uchaguzi, aliishukuru serikali kwa kupatia Vunjo fedha za miradi ya maendeleo zaidi ya Sh. bilioni 3.7.

Mwenyekiti wa CCM Moshi Vijijini, Cyril Mushi, alisema Halmashauri ya Moshi yenye jumla ya vijiji 157, haina maofisa watendaji katika vijiji 40, hivyo masuala ya uwajibikaji na hitaji la kusomwa mapato na matumizi kwa wananchi ni tatizo.

Mushi pia alimwomba waziri huyo kuwasaidia wananchi wa Vunjo kupata halmashauri yao kutokana na jiografia na ukubwa wake ili wananchi wapate huduma muhimu kwa urahisi.




Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa ofisi za Kanda ya Kaskazini za Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) jijini Arusha. Ofisi hiyo ya kanda itahudumia mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 3.5/- zatengwa kuwezesha mikopo kwa wanawake na vijana

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

TAASISI ya EFTA inayojishughulisha na utoaji wa mikopo ya mashine na magari bila dhamana kwa wajasiriamali na wakulima nchini, imetenga zaidi ya Sh. bilioni 3.5 kwa ajili ya kuwezesha vijana na wanawake kupata mikopo ya vifaranga vya kuku, chakula na mahitaji mengine.

Fedha hizo zitatolewa katika kipindi cha miaka mitatu ijayo kwa makundi hayo maalum pasi na kuwapo masharti ya dhamana.

Jana, Mkurugenzi Mtendaji wa EFTA, Nicomed Bohay, alitangaza neema hiyo jijini Arusha, wakati akitambulisha mpango huo wa mkopo wa kuku kwa wakazi wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini.

Kwa mujibu wa Bohay, mpango wa mkopo wa vifaranga vya kuku kwa vijana na wanawake wasiokuwa na ajira au wakulima wanaotaka kujipatia kipato cha ziada, ni wa kwanza na wa aina yake kwa taasisi za kifedha nchini kuutoa kwa wakopaji.

"EFTA imezindua mpango huu ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali ambayo imejipambanua kwa Watanzania kuhusu dhamira yake ya kuwainua kiuchumi vijana na wanawake.

"Kwa muda sasa, kundi la vijana na wanawake nchini limekuwa miongoni mwa makundi ambayo yanatajwa kuwa na idadi kubwa ya watu wasiokuwa na ajira rasmi, jambo ambalo limekuwa likichangia kuongezeka umasikini miongoni mwao.

"Serikali kupitia Mpango wa Jenga Kesho Bora, (BBT-YIA), imewezesha vijana wengi nchini kupata fursa ya mafunzo na mikopo ya kuanzisha na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kilimo na ufugaji nchini," alisema.

Kutokana na juhudi hizo za serikali, kampuni ya EFTA katika kuunga mkono jitihada hizo, nayo imeamua kuanzisha mpango wa majaribio wa mkopo wa kuku kwa vijana na wanawake bila dhamana.

Hatua hiyo inatajwa itawezesha makundi hayo kushiriki moja kwa moja katika shughuli za uzalishaji kupitia uwezeshwaji mkopo huo bila dhamana.

"Vijana na wanawake wengi hawakopesheki katika taasisi zetu za kifedha kwa sababu wengi wao hawana dhamana ya kuwawezesha kupata mikopo hiyo, ndio maana sisi baada ya kuiona changamoto hii.

"Tuliamua kuja na mpango wa kuwakopesha vifaranga vya kuku bila dhamana na tumechagua kuku kwa sababu uwekezaji wake ni wa muda mfupi na mkopaji ndani ya miezi michache anaanza kuona matunda ya uwekezaji wake," alifafanua.

Bohay aliongeza kuwa katika mwaka wa kwanza wa mpango huo, EFTA inategemea kutoa mkopo wa kuku 250,000 nchi nzima. Mpaka sasa wamekabidhi zaidi ya kuku 30,000 kwa wafugaji kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Meneja Masoko wa Silverlands Ltd, ambao ni wabia wa uzalishaji wa vifaranga hao, Mwanamvua Ngocho, alisema watahakikisha wafugaji wanapata vifaranga bora, chakula na chanjo ili kila mfugaji apate matokeo chanya kwa wakati.

Akizindua mpango huo, Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Arusha, anayeshughulikia Uchumi na Uzalishaji, Daniel Loroku, aliishukuru EFTA na Kampuni ya Silverland kwa kuja na mpango huu wa kusaidia vijana na wanawake kupitia mikopo ya vifaranga vya kuku bila dhamana.



# Wajawazito, watoto, wanaume wachangia wodi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

PAMOJA na wajawazito kulazimika kubeba ndoo za maji kwenda Kituo cha Afya Ushetu wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga kujifungua, wamejikuta katika fedheha ya kuchangia wodi moja na watoto na wanaume.

Licha ya ukosefu wa huduma hiyo, wajawazito, watoto na wanaume wanachanganywa katika wodi moja kutokana na uhaba wa majengo kituoni hapo.

Kilio hicho kimeibuliwa juzi wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme kwenye kituo hicho kukagua ujenzi wa wodi mbili zinazogharimu zaidi ya Shilingi milioni 50 zilizotolewa na Serikali Kuu na michango ya wananchi.

"Tunashukuru serikali kwa kuona kero hii na kutujengea wodi kwani tulikuwa tukichanganywa katika wodi moja watoto, wajawazito wanasubiria kujifungua, waliojifungua na ilikuwa imekatwa katikati kwa ajili ya wagonjwa kinababa hali iliyokuwa inatufanya kushindwa kubadilisha nguo kwa kuwaogopa wanaume waliokuwa kando," alisema Leticia Damas, Mkazi wa Kata ya Ulowa.

Leticia alitaja kero nyingine kuwa ni kituo hicho kukosa maji ya uhakika na kulazimika kufika kupata huduma wamejitwika kichwani ndoo za maji, hasa wajawazito wanaosubiri kujifungua.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mbika, Faida Lutege, alisema hali hiyo imekuwa ikiwalazimu baadhi ya wagonjwa kuruhusiwa kurejea nyumbani kabla ya kupona.

Awali akitoa taarifa ya ujenzi huo, Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho, Dk. William Richard, wamejenga wodi mbili na kwamba ya watoto imekamilika na kuwekewa vifaa vyote.

Dk. Richard, alisema ujenzi wa wodi ya wanawake, umekamilika kwa asilimia 90 na kinachosubiriwa ni kuwekewa madirisha na milango.

"Tatizo ambalo halijapata ufumbuzi ni kukosa huduma ya majisafi na salama, watumishi, mashine ya mionzi (utral sound) na X-ray kwani wagonjwa wanalazimika kusafiri umbali mrefu mpaka hospitali ya wilaya kupata huduma, alisema na kuongeza kuwa: "Kwa sasa tuna mpango wa kuajiri watumishi wa muda ili kutatua shida ya watumishi."

Akizungumza baada ya kupokea taarifa, Mndeme ametoa siku 10 kuhakikisha ujenzi ya wodi ya wanawake unakamilika na kuanza kutoa huduma ili kuondoa na adha ya wajawazito, wazazi kuchanganywa na wagonjwa wengine wodi moja na kuagiza kujengwa kwa wodi ya wanaume.

Vilevile alimwagiza Meneja wa Wakala wa Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mhandisi Paschal Mnyeti, kuchimba kisima kituoni hapo ili kuondoa tatizo la ukosefu wa maji.




Mhifadhi Misitu na Ofisa Nyuki wa Wilaya ya Kahama, Martha Machibya, akikabidhi funguo za pikipiki ya kubebea mizigo iliyotolewa na Barrick Buzwagi kwa katibu wa kikundi cha wafuga nyuki cha Mwendakulima, Rehema Juma, katika hafla iliyofanyika Kata ya Mwendakulima, wilayani Kahama jana. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano ya Jamii wa Mgodi huo, Stanley Joseph. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makanisa yawaombea waathirika Hanang'

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

UMOJA wa Makanisa ya Kipentecoste (CPCT) mkoani hapa umefanya ibada maalumu kuwaombea waathirika wa mafuriko wilayani Hanang' Mkoa wa Manyara huku ukitaka janga hilo kuwa fundisho kwa Watanzania.

Mwenyekiti wa Umoja huo, Askofu wa Kanisa la Voice of Salvation and Healing Church (VOSH), Joshua Wiliam akiongoza ibada hiyo kwenye Kanisa la PFCT mjini Geita, alisema kuwa tukio hilo limetikisa nchi nzima.

Askofu William, alisema Taifa limepoteza nguvu kazi kubwa katika tukio hilo, hivyo umoja huo unaungana na Watanzania kuwaombea majeruhi wapone haraka na waliofariki dunia wapumzike kwa amani.

Alisema tukio hilo halitasahaulika katika kumbukumbu za Watanzania, hivyo linatakiwa kuwa funzo katika kuzingatia maelekezo ya serikali kwa wanaoishi kwenye maeneo hatarishi ya mabondeni kuhama na wazazi na walezi kuwachunga watoto wao wakati mvua zinaponyesha ili kuepusha maafa.

"Tunamwomba Mungu mvua iendelee kunyesha, lakini atukinge na majanga haya, pia kwa jamaa waliowapoteza ndugu zao na kupitia katika kipindi kigumu cha majozi Mungu awatie nguvu na kuwajalia moyo wa uvumilivu," alisema.

Askofu wa Kanisa la PFCT Jimbo la Geita, Davidi Nzumbi, aliwataka waumini hao kujiandaa kiroho kwani hakuna anayejua lini na wapi siku yake ya mwisho itakapomkuta.

"Hili ni funzo kwetu kila mmoja anapaswa kujiandaa kiroho kwa maana hakuna anayefahamu siku wala saa, Watanzania wenzetu huko Manyara wametangulia mbele za haki hakika hawakufahamu Mungu awatie nguvu ndugu na jamaa zao," alisema Askofu Nzumbi.

Hadi kufikia juzi, takwimu zilizotolewa zinaonyesha kuwa waliokufa kutokana na maporomoko ya matope kutoka katika Mlima Hanang' walikuwa wamekufikia 89.

# SHUWASA yakarabati madarasa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) imekarabati vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Msingi Jomu.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi madarasa hayo juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa SHUWASA, Mhandisi Yusuph Katopola, alisema kama wadau wa elimu wana jukumu la kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira mazuri.

Katopola, alisema wamekarabati madarasa hayo kwa kuziba nyufa na kuweka sakafu ili kunusuru maisha ya wanafunzi na kuvutia mazingira ya kusomea.

"Tuna imani baada ya ukarabati huu na kufanya madarasa kuwa nadhifu na rafiki kwa wanafunzi, watasoma katika mazingira rafiki kabisa na kufanya vizuri kitaaluma," alisema Mhandisi Katopola.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Pendo Peter, alishukuru mamlaka hiyo kwa ukarabati madarasa hayo, hali ambayo itachangia wanafunzi kuendelea kufanya vizuri kitaaluma na kusoma bila wasiwasi.

Alisema Serikali imetoa fedha kwa ujenzi wa madarasa mengine matano kwa lengo la kuondoa msongamano wa wanafunzi.


**Tuna imani baada ya ukarabati huu na kufanya madarasa kuwa nadhifu na rafiki kwa wanafunzi, watasoma katika mazingira rafiki kabisa na kufanya vizuri kitaaluma.**

ama
ALHAMISI DESEMBA 14, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**MRADI MAJI VICTORIA KUTOMFIKIA... Mama Msalala hajatua ndoo; homa matumbo, UTI, mabinti watoro shule**



**PROF. JAMES SHABA 1935- 2023**
**Alihusudu kuhudumia kanisa, fani ya kaka ikamgeuza bingwa wa tiba**

Ukurasa 14

AFYA NA MIAKA 62 YA UHURU

# Dk. Samia alivyowekeza mtaji Sh. Tril.6.7 kwenye afya, MMAM hadi kupata bingwa

- Mwaka ujao shule 600, 92% ya waombaji
- Vituo afya ‘full nondo’ vifaa vimetimia
- Urafiki hospitali binafsi; bima afya rasmi

**Na Mwandishi Wetu**

TANGU aingie madarakani, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, staili ya uwekezaji wake katika maendeleo, eneo mojawapo ni katika afya chini ya kivuli cha Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi Tanzania (MMAM), wenye miaka 16 sasa.

Sura ya wazi ni katika mkakati wake aliyoutangaza mara tu alipoingia madarakani kuwa Rais, Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Sasa Rais ameitia saini na kuwa sheria kamili.

Ufafanuzi kuhusu uwekezaji huo, unapatikana kwenye maelezo ya Naibu Waziri wa Afya Dk. Godwin Mollel, akisema Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dk. Samia, imewekeza kwenye afya kwa kiasi kikubwa, ili kuhakikisha afya za wananchi zinaimarika

Dk. Mollel anayemwakilisha Makamu wa Rais katika Uzinduzi wa Chuo cha Afya Litembo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma, anasema hadi sasa, Rais Dk. Samia, amewekeza zaidi ya Sh. trilioni 6.7 katika afya.

Anafafanua kwamba, hizo ziko kwenye miundombinu, upatikanaji dawa, hata vifaa tiba, watumishi wa afya pamoja na ufadhili wa masomo kwa wataalamu afya, kupitia programu iitwayo Samia Scholarship.



Madaktari bingwa wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) na wenzao wa Shirika la Cardiostart International la nchini Marekani, wakimfanyia mgonjwa upasuaji mkubwa wa kubadilisha valvu ya moyo, ambao ni hatua mpya nchini katika mageuzi ya utaalamu wa afya. **PICHA: MTANDAO.**

“Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Dkt. Samia amewekeza zaidi ya Sh, bilioni nne, ili kuhakikisha wananchi wa Mbinga wanapata huduma bora za afyai,” anatamka Dk, Mollel, ambaye kitaaluma ni tabibu wa binadamu

Aidha, anasema rais Dk, samia, ameendeleza ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi, kuhakikisha sekta binafsi nayo inafanya vizuri katika afya nchini.

“Leo nipo hapa Litembo katika uzinduzi wa Chuo cha Afya Litembo, hii ni sehemu mojawapo ya serikali kuendelea kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi nchini,”anatamka Dk. Mollel

Anasema, katika mwaka uliopo unaoishia, serikali imenunua magari ya kubeba wagonjwa 727, ili yapelekwe kwenye maeneo yenye uhitaji kuhudumia wagonjwa.

Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, Aziza Mangosongo, anakitaja Chuo cha Afya Litembo, ni msaada mkubwa sana kwa wananchi wa mkoa Ruvuma na jirani, kwani inawazalisha wataalamu wengi wa afya.

**MITAJI YA RAIS**

Alipokuwa wilayani Njombe mwaka huu, Dk. Samia, akatangazwa kuwekeza katika Huduma za Dharura (EMD) 80 na Huduma za Wagonjwa mahututi (ICU) 28 zikiwapa huduma kwa wananchi.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Charles Mahera, anataja kuwa Jengo la Wagonjwa wa Dharura katika Hospitali ya Wilaya Makete ni miongoni mwa majengo 80 yaliyojengwa chini ya uwekezaji wa Rais Dk. Samia

Pia, Dk. Mahera anawataka maofisa ustawi wa jamii na lishe kutoa elimu ya makuzi ya watoto, kwa kuzingatia utamaduni, miongozo na elimu ya lishe, ili kuondoa udumavu katika maeneo yao, pia wakikabili magonjwa ya milipuko, jambo ambalo ni ajenda muhimu kwa Rais.

Dk. Mahera anasema:“Hivi sasa vifaa vingi serikali imewekeza katika ngazi ya msingi hivyo ni wakati wa kushirikiana hospitali za mikoa, kuwajengea uwezo watumishi wa ngazi ya msingi, ili vifaa vilivyowekezwa, kuleta tija kwa kutoa huduma kwa wananchi.”

Huku akikumbusha wajibu wa kufanyika ukaguzi katika hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati kuangalia usahihi wa dawa, vifaa tiba na ubora wa huduma, ili kuendana na uwekezaji uliofanyika katika maeneo yao.

Dk. Mahera ameelekeza wanganga wakuu wa wilaya nchini, kusimamia kwa karibu waratibu programu kama mifuko ya kimataifa na kuhakikisha fedha zake zinatumika kama zilivyopangwa, ili ku-

Inaendelea Uk. 14

AFYA

### MRADI MAJI VICTORIA KUTOMFIKIA…

# Mama Msalala hajatua ndoo; homa matumbo, UTI, mabinti watoro shule

**Na Shaban Njia, KAHAMA.**

UKOSEFU wa huduma ya Majisafi na Salama maeneo ya vijijini, unabaki kuwa mzizi wa tatizo kusababisha wananchi kuendelea kutumia maji machafu kila kukicha, hata kukaribisha magonjwa ya mlipuko.

Hapo kunatajwa magonjwa UTI na homa ya matumbo (typhoid), yakiwapata zaidi kinamama, watoto na wanafunzi shuleni, pia kuna maradhi ya kuharisha damu.

Mzizi unatajwa kunaanzia kwenye matumizi ya maji kutoka visima vifupi walivyochimba kwenye makazi yao na madimbwi yanayosadikiwa kutumika kwenye uzalishaji mpunga.

Katika kata ya Busangi Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, wakazi wake wanakabiliwa na shida hiyo kukosa majisafi na salama, huku wakati wa kiangazi, maji yao visimani yanakauka.

Ili kupata maji safi, wanalazimika kuamka alfajiri kwenda kuchota kwenye kata jirani za Ngaya na Masabi, ambako kumemepitiwa na Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria na wengi wanaambatana na mabinti, baadhi wanafunzi wa Shule ya Msingi Busangi, imeshawaathiri mahudhurio yao.



Wakazi wa Msalala, wilayani Kahama, wakiwa kwenye harakati za kuhangaikia huduma za maji. **PICHA: MTANDAO.**

**WAKAZI BUSANGI**

Lucy Manyeri anayesishi kata ya Busangi - Msalala, anakiri kuwapo shida ya huduma za majisafi na salama, hata wanalazimika kutumia yasiyo salama kwenye visima vyao, ambayo wakati wa kiangazi navyo vinakauka.

Ni uhaba anaoutaja kuwa chanzo cha magonjwa tajwa, akisema wanayafuata umbali wa kilometa 10, mifumo rasmi ya maji ya kiserikali na wanaamka alfajiri.

"Njiani tunakutana na masahibu mengi hasa ya kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia, ubakaji na kushambuliwa na wanyama aina ya fisi na kata ya Ngaya ina fisi wengi, kwa sababu ya mapango," anaeleza.

Mwingine Selina Samwel, anasema kwa sasa wanalazimika kununua kwa bei maji ndoo moja lita 20 Sh. 500 na kwa wasiokuwa na uwezo, wanafunga safari kusaka maji huko mbali, hivyo anaelekeza ombi, mamlaka ya maji- RUWASA, ifikirie kuwasogezea huduma ya maji kijijini Nduku-Busangi.

**MWALIMU/MTENDAJI KATA**

Msafiri Yohana, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Busangi, anaeleza kukosekana majisafi na salama, kunawasababishia utoro wanafunzi wao, hasa wasichana wanaoshirikiana na wazazi na walezi kutafuta maji alfajiri, hata siku za masomo.

Anasema, shule hiyo ina wanafunzi 1,251, mabinti wanaoongoza kwa utoro huo, kulinganisha na wavulana, kwa sababu wanashirikiana na wazazi kutafuta maji kwenye kata za jirani za Ngaya na Masabi.

Mwalimu Busangi anasema, ni hali inayowafanya kushindwa kufanya vyema masoma yao hususani Hisabati na kiingereza.

Aidha, anasema mabinti wanaongoza pia kwa kuugua UTI, kwa sababau ya uchafu wa vyoo shuleni mzizi chanzo kikuu kikiwa ni kukosekana maji, hivyo anauomba Mradi wa Maji Nduku-Busangi unaotekelezwa sasa, ukikamilika shule yake ipewe kipaumbele kuwasaidia wanafunzi masomoni.

**VIONGOZI MSALALA**

Ofisa Mtendaji wa Kata Msalala, Mathius Selemani, anasema wananchi wanatumia maji ya visima asili, vingi wamevichimbwa bila ya kutumia utalaamu, kipindi cha kiangazi vinakauka na wakati wa masika vinajaa maji, ndio wanayotumia sasa.

"Tuna kisima kimoja ambacho kinatoa huduma ya majisafi na salama na kilichimbwa miaka ya nyuma sana, ndicho ambacho hakikauki maji, iwe kiangazi na masika.

"Kulingana na wingi wa uhitaji wa maji, yamekuwa ya kugombania, hali inayofanya wengi kutumia ya kwenye visima walivyochimba wao," anafafanua Selemani.

Ofisa Mtendaji huyo anasema kata yake ina wakazi 14,890 wanaounda kaya 1,840, wote wahitaji wa maji. Anaiomba serikali wakati inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya maji, kuwapo mbadala wa kuchimbwa visima virefu, ili wananchi wawe na nafauu, wakati wanasubiri miradi hiyo mipya.

Diwani wa Kata ya Msalala, Alexander Mihayo, akikiri kuwapo tatizo kubwa la maji, akisema amekuwa akitumia vikao vya Baraza la Madiwani, kuwasilisha hoja za kilio cha maji, akisema katika mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, unaotekelezwa Nduku-Busangi, una ukubwa tanki lita 100,000.

Mbunge wa Msalala, Iddi Kassim, anasema amekuwa sehemu ya mapambano bungeni, kuhakikisha wananchi wake wanapata maji safi na salama na hivi karibu wamepokea Sh. bilioni 12 za kupeleka maji kwa wananchi vijijini.

Anasema, utekelezaji wa miradi ya maji unaendelea katika vijiji vya Mwazimba, Mwashigini, Buyange, Ilogi, Bulyanhulu na kata ya Ikinda.

**MENEJA RUWASA;**

Kaimu Meneja wa RUWASA-Kahama, Mhandisi Paschal Mnyeti, anakiri kata hiyo kukosa maji safi na salama na wananchi wake wanatumia maji ya visima asilia, ndio sababu ya kumeanzishwa wa mradi wa maji Nduku-Busangi unaotarajiwa kuhudumia zaidi ya wakazi 11,630 utakapokamilika Julai, mwakani.

Anafafanua, mradi utakuwa na awamu mbili za utekelezaji wake, awamu ya kwanza utakamilika mwishoni mwa mwezi Desemba na itahudumia vijijini vya Busangi, Nyamigege na Nduku.

Pia, inatajwa awamu ya pili ni ya vijiji vya Gulla, Ntobo, Masabi na eneo la makao makuu ya Halmashauri ya Msalala, mwakani 2024.

Anasema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 walitumia Sh.bilioni 21.5 kutekeleza miradi ya maji 14 na kati ya hiyo, miradi 10 ya Sh. bilioni 5.7 imekamilika, sasa inatoa huduma.

Mnyeti anasema, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, wamepokea Sh. milioni 322 ya kufanya utafiti wa maji na kuchimba visima virefu katika vijiji 20 vya Halmashauri ya Ushetu, vijiji vinane ni vya Msalalala, akiwahimiza makandarasi kukamilisha miradi iliyobaki kwa wakati.

"Mwaka jana mwezi julai hadi septemba tulitekeleza miradi 14 ambapo Msalala ipo miradi sita, Ushetu mitano na Manispaa ya Kahama miradi mitatu. Kati ya hiyo 10, imekamilika na inatoa huduma kwa wananchi.

AFYA

# Mkurugenzi OSHA aorodhesha mapinduzi afya kazini, sekta isiyo rasmi nayo mdau

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Usalama wa Afya Mahali pa Kazi (OSHA), hadi sasa inajivunia kuongeza Watanzania wanaojiajiri na kuajiriwa, ndani na nje ya nchi katika kipindi cha miaka mitatu, katika Serikali ya Awamu ya Sita.

Mkurugenzi Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, anasema utafiti wa mwaka 2021, uliofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO), nguvukazi ya Tanzania ina watu zaidi ya milioni 25, asilimia 55 wakiwa vijana, wengi wamejiajiri sekta isiyo rasmi.

Anasema, sekta hiyo ina vihatarishi vingi zaidi kazini kuanzia kifizikia, kibiolojia na majukumu ya kimakenika, akiendelea: "Wahusika katika sekta isiyo rasmi, wanakabiliwa na changamoto nyingi, ikiwamo uelewa mdogo wa masuala ya usalama na afya, hususani kutokutambua vihatarishi na athari zake na mbinu za kudhibiti."

Anasema, OSHA imeanzisha programu ya kuwahudumia wajasiriamali katika sekta isiyo rasmi, ili kuwajumuisha katika mifumo ya usimamizi wa usalama na afya kazini.

Khadija anasema, kupitia programu hiyo, wakala umewafikia hasa wanawake wajasiriamali wenye viwanda vidogo, vikundi vya wenye ulemavu, vijana na wachimbaji wadogo migodini nchini.

Anaitaja kaulimbiu yake "Afya yangu Mtaji Wangu" inajumuisha utoaji mafunzo na ugawaji vifaa kinga kwa wajasiriamali wadogo, kwa gharama ya OSHA.

Mkurugenzi huyo anataja katika kipindi hicho, wajasiriamali 37,803 wamepewa mafunzo ya usalama kazini, vifaa kinga, maeneo yao kukaguliwa, pia wana wataalamu afya wao.



Elimu ya afya kazini ikiendelea kutolewa. **PICHA: MTANDAO.**

Khadija anafafanua, awali usimamizi usalama na afya kazini ulikuwa chini ya Idara ya Kazi, kitengo kitwacho 'Ukaguzi wa Viwanda', lakini mabadiliko ya kisiasa, teknolojia, pia utandawazi na ukuaji uchumi, kulikoibuka vihatarishi vipya kazini, umeleta mabadiliko ya kisekta kazini.

**MABADAILIKO YALIVYOTOKEA**

Khadija anafafanua, zao lake ni kufanyika mapitio ya Sheria ya Ukaguzi wa Viwanda na kubaini maboresho mapya, baadhi ya mapungufu yakitajwa ni sheria kuusimamia usalama pekee kazi na kutozingatia athari za kiafya kwa wafanyakazi.

Mengine anayataja, sheria haikuzingatia ubora wa huduma inayotolewa, mafunzo, uhamasishaji na utunzaji takwimu za usalama na afya, akisisitiza msingi wa kujenga utamaduni wa kujikinga, pia hatari ya kutokea magonjwa, ajali na vifo kazini.

Anasema hivi karibuni, mabadiliko yaliyofanywa kwenye mifumo ya wizara, uwekezaji umepewa kipaumbele na kuhamishiwa Ofisi ya Rais.

Khadija anaitaja OSHA ni taasisi wezeshi, ikiwa na jukumu la kuhakikisha uwekezaji na tija kitaifa unakuwa, wananchi wananufaika kulinda nguvukazi ya taifa, ili kuwa na uzalishaji endelevu.

Anaeleza, wameshasimamia katika sura ya maboresho, kuondoa na kupunguza ada za huduma mbalimbali, ikijumuisha za usajili kazini, iliyoitozwa kati ya Sh. 50,000 hadi shilingi milioni 1, 800,000, ada ya fomu ya usajili kazi iliyotozwa shilingi 2,000 na kufuta faini za ukosefu wa vifaa vya kuzima moto, shilingi. 500,000;

Nyingine ni ada zilizofanyiwa maboresho ni: Leseni ya ithibati, shilingi 200,000 kwa mwaka; ushauri kitaalamu wa usalama na afya, shilingi 450,000; mafunzo ya elimu kwa umma, shiligi 250,000 kwa kila mshiriki.

Vilevile, imepunguzwa ada ya uchunguzi wa ajali iliyotozwa shilingi 500,000, sasa shilingi 120,000 pia anataja inagusa kipimo cha mzio na upumuaji.

Mengine anayataja ni kupunguzwa ada ya huduma za ukaguzi wa mifumo ya umeme katika vituo vya mafuta vijijini, kutoka shilingi 650,000 hadi shilingi150,000, kukilengwa kuhamasisha uwekezaji katika maeneo hayo, pia kupunguza athari.

Pia, kwenye vituo vya mafuta kumeondolewa ada ya ukaguzi wa usimamiziwa wa pampu za gesi kwa kila kituo cha mafuta.

Anasema, baada ya kufuta ada hizo, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akapendekeza bajeti zaidi ya shilingi bilioni 35, zitumike kuimarisha mifumo ya kulinda wafanyakazi, ili wawe na tija.

**ZAMA ZA TEHAMA**

Khadija anasema, OSHA imeshasimika Mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kuhudumia na kusimamia taarifa za ukaguzi nchini, kubaini ajali na kutoa mafunzo.

Anasema, TEHAMA imefanikisha kazi zao, ikipunguza muda wa kupata cheti cha usajili wa sehemu za kazi kutoka siku 14 hadi siku moja, ikifanya kwa njia ya kieletroniki.

"Mteja anaweza kuwa na uwezo kupata cheti chake cha usajili popote alipo, kutoa leseni ya ithibati ya usalama na afya mahali pa kazi, kutoka siku 28 hadi saba kwa sasa," anasema.

**YANAYOJIRI MAKAZINI**

Khadija anasema, OSHA sasa inashiriki katika miradi ya kimkakati, kama vile ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere wilayani Rufiji, mkoa Pwani, pia reli ya kisasa SGR, bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Tanga na upanuzi wa bandari nchini.

Vilevile inatajwa kupiga hatua, Tanzania imetambuliwa na mashirika kimataifa na nchi nyingine duniani, kuwa na mifumo bora ya usimamizi wa usalama na afya kazini.

Anaitaja kuvutia baadhi ya nchi Afrika, zikiwamo Kenya, Zimbabwe na Lesotho kuleta maofisa wake nchini kujifunza mifumo iliyopo.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, msimamizi wa Dawati la Usalama na Afya kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), kwa sasa ni mtumishi kutoka OSHA.

Anasema, serikali imeelekeza kuongeza fursa nyingine za ajira katika sekta rasmi na isiyo rasmi zisizopungua milioni saba, katika kipindi cha miaka mitano kwa taasisi ikiwamo OSHA.

Khadija anataja majukumu mengine ya OSHA ni kuchunguza ajali kazini na kushauri namna bora ya uzuiaji endelevu, akiambatanisha na takwimu za kupungua sasa.

Anataja baadhi; kufika asilimia 66.2 kutoka ajali 6,318 hadi 2,138 kwa kipindi hicho, huku waajiri 2,948 wakichukuliwa hatua kisheria, wngine, 2,814 wakapewa notisi kuboresha mahali pa kazi

# UNFPA: NUSU YA MIMBA HAZIKUTARAJIWA, MIAKA 75 YAPIGANA...SUDAN, UKRAINE, GAZA

**Na Yasmine Protace**

HAKI za binadamu zinahitaji uhuru wa mwili kwa wote. Azimio la Kimataifa la Haki za Binadanu lilipitishwa na Baraza kuu la Umoja wa mataifa miaka 75 iliyopita.

Hivi karibu Mwakilishi wa UNFPA nchini, Bryan Schereiner, naye akazungumzia kuhusu Siku ya Haki za Binadamu.

Anaongeza kuwa, hata ahadi yake inatoa wito wa utu, uhuru, amani na usawa kwa wote, akifafanua: "Wakati watu kila mahali wanathamini maadili haya ya ulimwengu, katika maeneo mengi sana haki za binadamu zimezingirwa, huku wanawake na wasichana wakiathirika hasa."

Pia, anafafanua takwimu zinazotaja nusu ya mimba ni zisizotarajiwa; kila dakika mbili mwanamke hufa kutokana na ujauzito au kujifungua.

" Mwanamke mmoja kati ya watatu anakumbana na ukatili katika maisha yake, huku vitisho vikiongezeka kwa wale wanaoishi kupitia majanga ya kibinadamu,' anasema.

Ikirejewa, Azimio la Kimataifa la Haki za Kibinadamu na mikataba mingine ya kimataifa ya haki za binadamu, inasisitiza uhuru wa mwili ni haki ya msingi na watu lazima wawe na uwezo wa kuamua uhuru na kuwajibika kuhusu miili yao wenyewe, ikijumuisha kama,

> **"Katika muktadha wote wa kibinadamu, UNFPA inafanya kazi kutetea haki za wanawake na wasichana kupitia kanuni za pamoja za haki, usawa na huruma," anasema.**

lini na ni watoto wangapi watapata.

Anaongeza kuwa kutambua haki hiyo, ni pamoja na kuhakikisha kunapatikana taarifa na huduma bora za afya ya uzazi na uzazi, hata katika migogoro na majanga.

Mark anasema, haja ni kukomeshwa unyanyasaji wa kijinsia makazini, majumbani na mazingira mengineyo, vitendo kama ukeketaji na ndoa za utotoni, zinapaswa kukomeshwa.

"Duniani kote, UNFPA inasimama na wanawake na wasichana katika kudai haki yao ya kujitawala kimwili, na maisha ya uhuru na usawa," anasema.

Anasema, sasa wanafanya kazi na serikali, pia mashirika ya kiraia kuhakikisha sera za afya ya ngono na uzazi zinazingatia haki za binadamu na kuwiana na mifumo ya kitaifa na kimataifa ya haki za binadamu.

Hapo anatumia mfano, nchi za Kenya, Jamhuri ya Kyrgyz, Msumbiji na Tanzania, UNFPA imesaidia kuoanisha programu za uzazi wa mpango na kanuni za haki za binadamu.

Anaongeza kuwa nchini Kosta Rika, kulisaidia kuunda muswada mpya unaowalinda wanawake wajawazito dhidi ya unyanyasaji wa uzazi kabla, wakati na baada ya kujifungua.

Mark anasema, juhudi za UNFPA kuboresha ukusanyaji wa data zinasaidia kukabiliana na ubaguzi na kutoa mwanga kwa watu ambao kwa muda mrefu wamesalia bila kuhesabiwa.

Kwa mara ya kwanza, anataja nchi za Kambodia, Jordan, Mexico, Turkmenistan na Zambia, sasa zinakusanya takwimu za sensa ya watu wenye ulemavu, hatua ambayo ni muhimu kulinda haki zao.

Katika machafuko, UNFPA inatajwa kusimama na wanawake, wasichana na vijana walioko katika mazingira magumu, wenye jukumu muhimu katika kutafuta amani na usalama kwa kufanya kazi ili kuzuia, kushughulikia na kukabiliana na ukiukwaji wa haki.

"Katika muktadha wote wa kibinadamu, UNFPA inafanya kazi kutetea haki za wanawake na wasichana kupitia kanuni za pamoja za haki, usawa na huruma," anasema.

Anaongeza kuwa, huko kunakoendele[...] pigano sasa; Gaza, Sudan na Ukraine, U[...] inasambaza vifaa safi vya kujifungulia, [...] hakikisha uzazi salama na matunzo ba[...] kuzaa.

Anaongeza kuwa, wanawapa wanawa[...] wasichana waliohamishwa katika umri [...] zaa vifaa vya heshima ili kudumisha us[...] hihi na kukidhi mahitaji yao ya afya ya h[...]

Mark anaeleza kuwa, kwa miaka 75 [...] kupitishwa kwake, Azimio la Kimata[...] Haki za Kibinadamu, linakumbusha [...] wa kuchwa maadili yenye msingi au kup[...] mtazamo wa dunia unaotafutwa.



Mkuu wa UNFPA, Mark Bryan Schereiner. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

PROF. JAMES SHABA 1935- 2023

# Alihusudu kuhudumia kanisa, fani ya kaka ikamgeuza bingwa wa tiba

**Na Christina Mwakangale**

KWA mwonekano kimo chake cha wastani, mcheshi na mpenda kujichanganya na watu. Enzi za uhai wake, wamo wanoaomuelezea alivyojumuika nao kwenye maeneo tofauti ya kujiburudisha; daima hajikwezi, ila yatokonayo na mantiki yake yamemkweza.

Imepita wiki sasa tangu kifo chake, Prof. James Shaba, unazuru mitandao ya kijamii utabaini hilo, kwamba alikuwa anajichanganya na jamii, ingawa utambulisho mkuu ni ubingwa wa kufanya 'postmortem' hospitalini.

Mmoja wa wafuasi wa Nipashe digital mtandao wa Facebook, anasema: "Dah! Prof Shaba ni Yule aliyekuwa Muhimbili akichunguza miili ya watu waliokufa kitata? Au ni mwingine? Akajibiwa: "Ni huyo huyo."

Wenyewe wanazuoni wanamjua kwa utambulisho 'pathologist', elimu ya utabibu inmayozama katika sura ya kina ya mwili wa binadamu na mabadiliko yake ya asili.

Prof. Shaba, aliyejizolea umaarufu katika stadi ya kuutambua mwili wa binadamu na sababu za kifo, ameitumikia sana Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH),

Katika familia ya Shaba, amebeba tafsiri kuu ya 'maji kufuata mkondo'. Ndivyo anavyotafsiriwa Prof. James Shaba, Daktari Bingwa wa Tiba ya Binadamu, kuutambua mwili wa binadamu na sababu za kifo.

Tangu utotoni akiishi na kaka yake, John Shaba, mtaalamu mwandamizi wa Maabara Kuu ya Patholojia katika Hospitali ya Ocean Road, Dar es Salaam (sasa taasisi ya Kansa), mara kadhaa, hakusita kumuomba achungulie kilichomo katika darubini.



Profesa James Shaba

Familia ya marehemu Prof. Shaba, kupitia binti yake, Anale, inameuelezea wasifu wa bingwa huyo, aliyefariki dunia wiki iliyopita, huko Chicago nchini Marekani, akiwa na umri wa miaka 88.

Taarifa iliyotolewa na familia hiyo kwa Nipashe, juzi ilielezea kwamba shughuli za mazishi zinaendelea Marekani na maziko yake yanatarajiwa kufanyika Desemba 16, mwaka huu.

Prof. Shaba, aliyejizolea umaarufu katika stadi ya kuutambua mwili wa binadamu, pamoja na mkewe Elizabeth Shaba, walijaliwa watoto watatu; Anale, Stella pamoja na Dk. Hamish Shaba (marehemu).

Moja ya sifa, iliyomtangaza sana kipekee, kuwa ndiye daktari bingwa aliyefanyia uchunguzi mwili wa aliyekuwa Waziri Mkuu Edward Sokoine, aliyefatriki kwa ajali ya gari Aprili 12, 1984.

Inaelezwa, Prof. Shaba ni mzaliwa wa April 5, mwaka 1935 Sumbawanga mkoani Rukwa, akiwa mtoto wa mwisho, miongoni mwa watoto sita wa Mzee Edward Fusi Shaba na Mama Lucy Soko.

"Katika umri wake mdogo (Prof. Shaba), aliishi na kaka yake aliyeitwa John na familia yake. John alikuwa Mtaalamu Mwandamizi wa Maabara katika Maabara Kuu ya Patholojia Hospitali ya Ocean Road. Mara kwa mara akamruhusu Prof. Shaba mwenye shauku, kuchungulia darubini," ilisema taarifa hiyo.

Prof. Shaba, baadae akaamua kujikita katika fani ya afya hadi kuibukia daktari bingwa, licha ya kuwa na matamanio kuendelea na maisha ya kikanisa. Alihitimu masomo yake ya sekondari katika Shule ya Tabora Boys, akiwa chini ya ulezi wa Mama Mary Hancock, Mbunge.

Kisha mwaka 1962, Prof Shaba, akahitimu Shahada ya Kwanza ya Udaktari (Bachelor of Medicine and Bachelor of Surgery degree-MBCh.B), katika Chuo Kikuu cha Makerere, nchini Uganda.

Aliwahi kuajiriwa katika Hospitali ya Mwanamfalme Margaret Hospital, Dar es Salaam, Tanzania na mwaka 1965, Prof. Shaba akaenda kwenye Chuo Kikuu cha Glasgow huko Scotland, Uingereza, alikohitimu shahada ngazi ya juu ya udaktari wa falsafa (Ph.D) katika Patholojia ya Uchunguzi.

Mwaka 1969, akasajiliwa kama daktari katika Maabara Kuu ya Patholojia nchini Tanzania na mwaka 1970, Prof. Shaba, alikuwa mwanachama wa Chuo cha Patholojia Royal, London, Uingereza.

Baada ya kuhitimu Shahada yake ya Uzamivu, Profesa Shaba akatumikia taaluma yake kama daktari bingwa wa magonjwa na mhadhiri katika Hospitali ya Glasgow Royal Infirmary, kabla ya kurejea Tanzania.

Akiwa nchini, Prof. Shaba, akafanya kazi katika Wizara ya Afya, Chuo Kikuu Dar es Salaam (UDSM) na Chuo cha Afya Muhimbili, baada ya kujitenga. Pia, alihudumu katika Chuo cha Afya cha Helsinki, nchini Finland.

Akastaafu kazi, baada ya kutumia muda wote UDSM, Muhimbili katika Kituo cha Paholojia-Idara Kuu ya Histopatholojia na Anatomia. Kadhalika, miaka ya 1990, akaendelea kujitolea na kushirikiana na sekta binafsi.

Famlia inasema, baada ya maziko, chochote kitakachosalia, baada ya kuhitimisha gharama za mazishi, fedha itakayosalia itaelekezwa katika taasisi ya Cook County Health Foundation, iliyoko Chicago, Marekani, kuendeleza fikra zake za kitaaluma.

AFYA NA MIAKA 62 YA UHURU

# Dk. Samia alivyowekeza mtaji Sh. Tril.6.7 kwenye afya, MMAM hadi kupata bingwa

**Inatoka Uk. 11**

leta tija kwa wananchi.

**MABINGWA WANAZALISHWA**

Simulizi ya kunoa madaktari kupata matabibu bingwa ndani yao, ni hivi karibuni Rais Dk. Samia akaidhinisha pesa, Sh. Bilioni tisa kwa ajili ya kusomesha wataalamu bingwa na wabobezi 601 wa fani mbalimbali za afya, kuongeza idadi ya wataalam wa kada hiyo nchini.

Waziri wa Afya. Ummy Mwalimu, akitamka wiki kadhaa sasa kwamba nchini, ili umma upate huduma yao kwa wingi na ufasaha, kilichofanyika safari hii ni kwa ajili ya mwaka wa fedha 2023/24.

"Fedha hizo ni muendelelezo wa uwekezaji mkubwa unaofanywa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan," anatamka Waziri Ummy, akisema ni ferdha zianazowaangukia wataalamu wapya 601 sawa na asilimia 92 ya waombaji waliokidhi vigezo vya kusomea utaalamu wa ubingwa na bobezi wa fani mbalimbali za sekta ya afya.

"Ufadhili huu ni kwa ajili ya kulipiwa ada ya mafunzo na posho ya utafiti kwa watakaofadhiliwa ndani ya nchi na kwa wanaoenda kusoma vyuo vya nje ya nchi watalipiwa ada, posho ya kujikimu wakiwa masomoni (Stipend), nauli ya kwenda na kurudi pamoja na posho ya utafiti," anasema Waziri Ummy.

Hapo Waziri anawataka wataalamu wote waliopata ufadhili huo wa mwaka 2023/2024, kukamilisha taratibu za kujaza mikataba ya ufadhili kama ishara ya kuukubali.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, muda wa kujaza mikataba ya ufadhili ni kuanzia Novemba 29, 2023 hadi juzi Desemba 12.



# NBS yafanya utafiti sekta kilimo, upatikanaji huduma za kijamii

**Na Thobias Mwanakatwe,**

SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amezitaka kaya zilizochaguliwa mkoani mwake zitakazoshiriki utafiti unaofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), kutoa ushirikiano kwa makarani na wadadisi ili kupata taarifa sahihi.

Utafiti huo utagusa maeneo ya kilimo, uchumi na jamii.

Utafiti huo pia unalenga kufanya tathmini ya upatikanaji endelevu wa huduma za maji, elimu ya afya na usafi wa mazingira.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Serukamba alisema NBS imeanza utafiti wa sekta hizo ili kuiwezesha nchi kupata takwimu zitakazotumika katika kutunga na kuhuisha sera, kupanga mipango, programu za maendeleo, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wake.

Serukamba alisema katika utafiti wa kilimo wa mwaka 2022/23, watafuatilia maendeleo ya sekta ya kilimo nchini kwa kukusanya taarifa kuhusu hali ya kitaifa ya uzalishaji mazao, idadi ya mifugo na mazao yatokanayo na mifugo, utoaji wa huduma na matumizi ya rasilimali ili kuongoza utekelezaji wa sera na mipango ya serikali kuhusu sekta ya kilimo.

"Utafiti huu wa kilimo ni muhimu sana kwa kuwa sekta ya kilimo inachangia wastani wa asilimia 26.2 ya Pato la Taifa, inatoa ajira karibu asilimia 65 ya watu wote nchini, inatuhakikishia usalama wa chakula na ina mchango mkubwa kwa maendeleo ya sekta nyingine hususani sekta ya viwanda," alisema.

Kuhusu utafiti wa kutathmini upatikanaji wa huduma za maji, elimu ya afya na usafi wa mazingira 2023, Serukamba alisema utaisaidia serikali na wadau wa maendeleo kuelewa changamoto zinazokabili upatikanaji wa huduma hizo na kuchukua hatua stahiki za kuziimarisha, kuongeza upatikanaji wake na kuinua viwango vya ubora.

Serukamba alisema utafiti wa shughuli za kiuchumi na kijamii wa mwaka 2023, unafanyika ili kupata idadi ya shughuli za kiuchumi na kijamii zilizopo katika sekta iliyo rasmi na kupata muhimili wa sampuli ambao utatumika kama mwongozo wa watafiti mbalimbali.

Serukamba alisema chini ya Sheria ya Takwimu, wajibu wa mwananchi ni kutoa ushirikiano kwa wadadisi wa utafiti huu kwa kutoa majibu sahihi ya maswali yatakayoulizwa kwani hii si mara ya kwanza kwa wananchi wa Mkoa wa Singida kushiriki utafiti wa kitakwimu.

Meneja Takwimu Ofisi ya Taifa ya Takwimu Mkoa wa Singida, Naing'oya Kipuyo, alisema utafiti huo kwa mkoa huu ulianza Novemba mwaka huu ambapo makarani na wadadisi wamesambazwa katika halmashauri zote saba za Mkoa wa Singida.

Kipuyo alisema katika utafiti wa kilimo mwaka 2023, kaya 300 za kilimo zitahojiwa katika maeneo 25 na kwamba zoezi hilo litachukua miezi miwili.



Ofisa Utumishi Mwandamizi, Idara ya Uendelezaji Sera, Ofisi ya Rais-Utumishi, Judith Abdallah, akiwaelekeza washiriki wa Mafunzo ya Mfumo wa Upimaji wa Utendaji Kazi wa Watumishi Serikalini (PEPMIS) kutoka TANESCO, REA na EWURA jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 'TANESCO iimarishe huduma, izingatie maslahi watumishi'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amelitaka Shirika la Umeme (TANESCO) kuzingatia maslahi ya watumishi wake ili kuongeza ufanisi na ubunifu katika kutekeleza majukumu yao.

Katambi aliagiza hayo jana jijini hapa alipofungua mkutano wa Baraza Kuu la 53 la Wafanyakazi wa shirika hilo linalofanyika kwa siku mbili kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali ya kiutendaji.

Alisema ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa watumishi ndani ya shirika hilo, maslahi ya watumishi yanapaswa kupewa kipaumbele ili kuongeza uwajibikaji.

"Ili kuongeza ufanisi wa shirika letu hili, ambalo tunalitegemea katika uzalishaji wa umeme, mnapaswa kuzingatia maslahi ya watumishi wenu kwa kuwapa motisha, posho, kupandishwa vyeo ili kuwaondolea msongo wa mawazo watumishi na kuongeza tija na ubunifu katika shirika hili," aliagiza.

Katambi pia aliwataka watumishi wa shirika hilo kuzingatia wajibu wao katika utekelezaji wa majukumu kabla ya kudai haki zao.

"Kabla ya kudai haki zetu lazima tuangalie wajibu wetu katika maeneo yetu tumeutimiza kwa ukamilifu. Suala la umeme nchini ni jambo la muhimu sana, hivyo tunapaswa kutimiza majukumu yetu ili kuondoa malalamiko ya mgawo wa umeme nchini," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Gissima Nyamo-hanga alisema mkutano wa baraza hilo utafanyika kwa siku mbili ukiwa lengo la kujadiliana mambo mbalimbali ya kiutendaji.

Vilevile, alisema maagizo yote yalitolewa na Naibu Waziri Katambi watayafanyia kazi ili kuongeza ufasi katika utekelezaji majukumu mbalimbali kwa watumishi wao.

"Baraza Kuu la Wafanyakazi ni chombo ambacho majukumu yake ni kuangalia maslahi na haki za wafanyakazi. Katika kikao chetu pia tutakwenda kujadili masuala ya maslahi kwa watumishi na haki zao," alisema.

# Majaliwa, Balozi Saudia wateta uwekezaji nchini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekutana na Balozi wa Saudi Arabia nchini, Yahya Ahmed Okeish na kujadiliana masuala mbalimbali yakiwamo ya kilimo, uvuvi na uwekezaji.

Akizungumza na balozi huyo jana ofisini kwake, Mlimwa jijini Dodoma, Waziri Mkuu alisema anatambua matunda ya uhusiano wa muda mrefu ambayo Tanzania imeyapata kutoka Saudi Arabia ikiwamo misaada kwenye sekta za afya, elimu na maji.

"Natambua dhamira ya Saudi Arabia kuja kuwekeza kwenye kilimo, wakiwa tayari tutawapokea na natumaini watatumia vizuri fursa hiyo kuendeleza kilimo. Lakini tunazo fursa za uwekezaji za uvuvi kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Nitumie fursa hii kukaribisha kampuni za Saudi Arabia zije kuwekeza kwenye uvuvi wa bahari kuu kwani huko kuna samaki aina ya tuna," alisema.

Majaliwa aliishukuru nchi hiyo kwa kukubali kununua nyama kutoka Tanzania na akatumia fursa hiyo kuwaomba waongeze wigo wa kununua nyama zaidi na kuwahakikishia kwamba Tanzania itaendelea kuwapatia nyama yenye viwango bora.

Aliipongeza serikali ya nchi hiyo kwa uamuzi wake wa kuanzisha safari za moja kwa moja kutoka Saudi Arabia hadi Tanzania kwa kuwa zitasaidia kuimarisha utalii na watu wanaokwenda Hijja.

"Ninayo taarifa kwamba hivi karibuni, Shirika lenu la ndege litaanza pia safari za moja kwa moja kutoka Saudi Arabia hadi Zanzibar. Hii si tu kwamba itasaidia kuongeza idadi ya watalii bali pia itawawezesha watu wanaoenda umra na hijja," alisema.

Wakati huo huo, Majaliwa alitumia fursa hiyo kumpongeza Mfalme wa nchi hiyo, Salman Bin Abdulaziz Al Saud na Waziri Mkuu wake, mwanamfalme Mohammed Bin Salman Bin Abdulaziz Al Saud kwa ushindi ambao nchi hiyo imeupata ili kuwa mwenyeji wa maonyesho ya kimataifa duniani ya Expo 2030.

Maonyesho hayo makubwa duniani, yanatarajiwa kufanyika jijini Riyadh kuanzia Oktoba, 2030 hadi Machi 2031. Saudi Arabia ilipata ushindi wa kura 119. Majiji mengine yaliyokuwa yakiwania nafasi hiyo ni Busan (Korea Kusini) na Roma (Italia).

Awali, Balozi Okeish alitoa pole kwa Serikali ya Tanzania kutokana na maafa makubwa yaliyotokea Katesh, Hanang mkoani Manyara na kupongeza jitihada zilizofanya kuokoa maisha ya walionusurika na kurejesha huduma kwa wananchi hao.

Alimweleza Waziri Mkuu kwamba amekutana na wafanyabiashara wengi wa Saudi Arabia ambao kwanza wamekubali kuja kutembelea Tanzania lakini pia wako tayari kuunda Baraza la Wafanyabiashara baina ya Tanzania na Saudi Arabia.



# Spika: Matumizi bora ya ardhi yatatatua migogoro

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MIKAKATI iliyowekwa na serikali, ikijumuisha miongozo ya matumizi bora ya ardhi kwenye vijiji, itasaidia kumaliza migogoro ya ardhi ikiwamo ya wakulima na wafugaji.

Spika wa Bunge ambaye ni Rais wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Akson, alitoa kauli hiyo juzi alipofungua mkutano wa 28 na maadhimisho ya miaka 30 ya Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) uliofanyika mkoani hapa.

“Tunatamani migogoro kati ya wafugaji na wakulima iishe nchi hii. Tunatamani migogoro ya ardhi iishe nchi hii, itatuchukua muda lakini hatua zimeshaanza kuchukuliwa kwa maana ya kwamba vijiji kupimwa na kupanga matumzi bora ya ardhi.

“Ardhi hii ikitengwa kwa ajili ya kilimo, basi ifanye kazi ya kilimo na asiwapo mkulima wa kupora au hata kama si mkulima, ni mfugaji, basi asiwapo mfugaji ambaye anaporwa ardhi yake.

“kwahiyo, mipango hiyo ipo na katika utekelezaji wa bajeti mwaka huu wa fedha (2023/24), fedha hizo zimetengwa, na tutaanza na baadhi ya maeneo,” alisema.

Dk. Tulia alisema huduma hiyo itakapoanza na MVIWATA watakuwa sehemu ya wafaidika kwa sababu changamoto ya wakulima na wafugaji pamoja na watu kuporwa ardhi itapungua.

Pia Spika Tulia aliwataka wakulima kuendelea kuzalisha sambamba na kuyapandisha thamani mazao yao kwa kuwa kufanya hivyo kutapanua soko la kimataifa na kuwa na uhakika na kilimo chao.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, alitoa rai kwa wakulima kwamba licha ya kuzalisha mazao kwa wingi, wakumbuke kuwaandalia watoto wao chakula ambacho kimeongezwa virutubisho.

“Kinamama na kinababa tunapozalisha bidhaa zetu za kilimo, tukumbuke kutenga mlo ulio bora nyumbani, mlo ulio bora hautoki nje, ni mboga za majani unazolima mwenyewe, ni parachichi unayolima mwenyewe ndiyo tunda, ni mahindi unayolima mwenyewe ndiyo wanga, kuku unayefuga mwenyewe ndiyo protini,” alisema Mtaka.

Mkurugenzi Mtendaji wa MVIWATA, Stephen Ruvuga, alisema baadhi ya changamoto zinazowakabili wakulima ni pamoja na kuwapo uporaji ardhi vijijini ambao unaathiri wakulima wadogo.

“Kuna migogoro mbalimbali ya ardhi, mingine ya wazi, mingine inayofukuta chini kwa chini katika maeneo mbalimbali ikiwamo migogoro kati ya wawekezaji na wakulima wadogo, wafugaji na wakulima, kati ya taasisi za serikali na wakulima na tunaamini ardhi ni uhai na si bidhaa, hivyo kama taifa lina kila sababu ya kuhakikisha ulinzi wa ardhi kwa wakulima wadogo,” alisema Ruvuga.

Mmoja wa wakulima aliyeshiriki mkutano huo, Sara Kinyunyu, aliiomba serikali kuwapa haki ya kumiliki ardhi ya kutosha ambayo ndiyo inawawezesha kuwa wakulima na si kuwapa kipaumbele wawekezaji pekee.

# Wapata mwarobaini wa kero za wakulima

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKULIMA wa mazao jamii ya kunde mkoani Njombe, wameshauri kuwa na mtandao utakaosaidia kurahisisha upatikanaji mbegu bora za mazao hayo na masoko ya uhakika ili kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Ushauri huo ulitolewa katika mkutano wa jukwaa la wadau wa mazao jamii mikunde kupitia mradi BEEP (Beans for Economic Empowerment Project) unaotekelezwa katika mikoa ya Njombe na Ruvuma, ukifadhiliwa na AMDT na kusimamiwa na taasisi ya BRITEN.

Baadhi ya wakulima hao walisema changamoto ya masoko na gharama kubwa ya mbegu itatatuliwa pindi tu wakiungana ili kuwa na kauli moja.

Mmoja wa wakulima hao, Yohana Mhagama alisema changamoto ya maharage ni bei na ushindani ulioko sokoni.

“Pili, kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kidogo uzalishaji unapungua na kuna magonjwa mengi kwa zao la maharage.

Kwa upande wa wanunuzi wa maharage lishe na wahamasishaji wa matumizi wa maharage lishe kutoka Taasisi ya BIVAC, akiwamo Beatrice Msafiri, walitoa rai kwa wakulima kuendelea kulima mazao hayo ili kupunguza changamoto ya afya kwenye jamii.




Wafanyakazi wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO) Mkoa wa Mbeya wakijiandaa kufanya kazi ya kuhamisha nguzo za umeme ili kupisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya njia nne katika eneo la Iwambi jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Tamaa ya fedha chanzo kufichwa taarifa za ukatili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wazazi na walezi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wanadaiwa kuendelea kuficha taarifa za vitendo vya ukatili dhidi ya watoto kutokana na uelewa mdogo pamoja na tamaa ya fedha.

Inaelezwa kuwa baadhi yao wamekuwa wanamalizana na watekelezaji vitendo hivyo kupitia kwenye vikao vya familia na wengine kulipwa fedha kwa makubaliano ya kutoendelea kufuatilia, jambo ambalo linasababisha vitendo hivyo kushamiri.

Wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia walieleza hayo walipofanya ziara katika Kijiji cha Izumbwe kilichoko Kata ya Igale kwa lengo la kuwaona wahitaji na kufanya usafi kwenye maeneo ya taasisi za umma.

Katibu wa Vituo vya Taarifa na Maarifa Wilaya ya Mbeya, Juhudi Mwajunga, alisema jana kuwa kumekuwa na ushirikiano hafifu baina yao na wazazi na walezi wa watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili.

Alisema wanapopata taarifa za mtoto yeyote kufanyiwa ukatili, wamekuwa wanafuatilia kwa lengo la kuwasaidia watoto hao, lakini ushirikiano wa wazazi umekuwa hafifu, hali ambayo inasababisha ushahidi kukosekana.

Alisema kazi yao ni kufuatilia vitendo hivyo, lakini vikwazo kutoka kwa baadhi ya wazazi na walezi kutoonesha ushirikiano vimekuwa vinasababisha watuhumiwa wa matukio hayo kutofikishwa mahakamani.

“Unakuta mtaani taarifa zipo kwamba mtu fulani amembaka mtoto fulani, lakini tukitaka kufuatilia tunapata vikwazo kutoka wa wazazi, hawatoi ushirikiano kabisa, lakini ukifuatilia unakuta familia zilishamalizana kwa kificho,” alisema Mwajunga.

Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Sauti ya Mama Afrika (SAMAFO), Tabitha Bugali aliwataka wazazi na walezi kuacha tabia ya kuficha matukio ya ukatili kwa maelezo kuwa wanawakosesha watoto haki zao.

Alisema utaratibu huo wa kuficha taarifa za wahalifu hao unachochea ongezeko la vitendo vya ukatili kutokana na watuhumiwa kutofikishwa kwenye vyombo vya sheria.

“Niwaombe wazazi na walezi hasa kinamama, msiogope kutoa taarifa za vitendo vya ukatili kwa watoto hata kama aliyefanya ni baba au ndugu wa karibu kwa sababu vitendo hivi havikubaliki,” alisema.



# Waziri amtwisha zigo mwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Muhammed Said amemtaka Mkurugenzi wa Changuu Lodge, Davide Azzola, kutangaza historia ya makumbusho katika Kisiwa cha Prison Island ili kuongeza idadi ya watalii visiwani hapa.

Akizindua makumbusho hayo, Waziri Simai, alisema yana historia kubwa kwa Zanzibar kwa miaka mingi, lakini watalii wamekuwa wakifika na kukosa historia yake kutokana na kutokuwapo.

Alisema kuwapo kwa makumbusho hayo kutasaidia watalii kujifunza historia yake kuwa kulikuwa na jela ya wahalifu sugu na watumwa wakati wa ukoloni.

Alimshauri Azzola ambaye ni mwekezaji wa kisiwa hicho kuhakikisha taarifa za historia ya makumbusho hayo zinazotolewa kwa watalii na wageni kwa lugha za mataifa mbalimbali duniani.

Akizungumzia kuhusu uwekezaji wa visiwa vidogo vilivyopo Unguja na Pemba, alisema Serikali ya Zanzibar (SMZ) imeamua kuongezewa tija zaidi.

"Mtazamo wa Serikali ya awamu ya nane ni kushirikiana na sekta binafsi kuyaendeleza maeneo mbalimbali, mwekezaji wa kisiwa hiki atakiendeleza kwa kujenga vyumba 50 na kuzalisha ajira 300 na kuwanufaisha wananchi kupitia biashara," alisema.

Alimpongeza mwekezaji huyo kwa ubunifu na kumtaka kuongeza huduma nyingine kwa wageni na kuhakikisha rasilimali zilizopo kisiwani hapo zinatunzwa.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), Sharif Ali Sharif, alisema katika mkataba baina yao, wamemtaka mwekezaji huyo kuhakikisha anakitunza kisiwa hicho na historia iliyokuwapo inaendelezwa.

Sharif, alisema kisiwa hicho ni muhimu kwa ajili ya kukuza uchumi wa Zanzibar na kuzitaka taasisi kutoa ushirikiano kwa mwekezaji huyo kwa kuwa ametumia gharama kubwa kuendeleza maeneo hayo.

"Tumezoea utalii wa fukwe pekee, lakini kwa sasa utalii umekua Zanzibar, kuna utalii wa makumbusho kwa ajili ya kutunza historia kwa manufaa ya vizazi vijavyo kujua historia ya nchi yao," alisema Sharif.

Aliwataka wawekezaji kuendelea kujitokeza Zanzibar ili kukuza utalii na uchumi visiwani hapa.

Akizungumza katika hafla hiyo, Azzola, alisema lengo la kuanzisha makumbusho hayo ni kuhakikisha wageni wanapata historia sahihi ya kisiwa hicho na kuongeza vivutio vya utalii Zanzibar.

## SMZ kuanza 2024 kwa utalii wa kijani

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), imepanga kuanza kufanya mkutano wa utalii endelevu wa kijani kulinda utajiri wa rasilimali za baharini na kupambana na mabadiliko ya tabia ya nchi..

Mpango huo ulitangazwa jana na Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Hafsa Faisal Mbamba wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano huo unaotarajiwa kufanyika mwanzoni mwa mwaka 2024.

Alisema tamko la Zanzibar kuhusu utalii endelevu umejikita kuchukua hatua stahiki katika sekta hiyo kwa lengo la kuinua pato la wananchi na taifa.

Alisema mkutano huo umezingatia matakwa ya kimataifa ikiwemo tamko la Glasco kuhusu mabadiliko ya tabia ya nchi kwenye sekta ya utalii na malengo endelevu ya maendeleo ya Umoja wa Mataifa ya Utalii unazingatia mazingira.

Katibu huyo, alisema mikakati ya SMZ kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na wawekezaji ni kuona sekta hiyo inaleta mageuzi makubwa ya kukuza utalii na kuepuka athari za mabadiliko ya tabia ya nchi.

Alisema hoteli za ukanda wa kaskazini na kusini mwa Unguja zipo katika hali mbaya kutokana na maji ya bahari kuvamia maeneo ya fukwe na kutishia uwekezaji katika maeneo hayo.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo, Dk. Ameir Omar Ali, alisema utalii endelevu unatakiwa kwenda sambamba na mikakati ya kulinda hifadhi za baharini na mazalia ya samaki na matumbawe ambayo yapo katika tishio la kutoweka.

Alisema kumejitokeza uvuvi haramu katika maeneo ya ukanda wa bahari ya Zanzibar ikiwamo matumizi ya nyavu zenye macho madogo ambazo ni hatari kwa kunasa samaki wadogo ambao hawafai kula huku matumbawe yakiathirika kwa kuvunjwa vunjwa.



Watendaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na wanarakati wa kupinga ukatili na udhalilishaji, wakiwa katika kilele cha maadhimisho ya kufunga siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia Muyuni, Wilaya ya Kusini Unguja juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Balozi alonga wanawake uongozi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BALOZI wa Norway nchini, Tone Tinnes amesema ukatili dhidi ya wanawake ni miongoni mwa vitendo ambavyo vinawakwamisha kufikia malengo yao ya kushika nafasi mbalimbali za uongozi.

Balozi Tinnes alisema hayo wakati wa mdahalo wa kitaifa wa wadau wa kutetea wanawake, uongozi na ushiriki wao katika demokrasia visiwani hapa ulioandaliwa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA) na Jumuiya ya Utetezi wa Jinsia na Mazingira Pemba (PEGAO) kwa kushirikiana na Ubalozi wa Norway nchini.

Akizungumza kwenye mdahalo huo uliolenga kujadili hali ya wanawake na uongozi nchini, alisema ajenda ya usawa wa kijinsia ni muhimu kutiliwa mkazo na wadau wote ili kuhakikisha inafikiwa bila kuwa na vikwazo vya aina yoyote.

Alisema ajenda ya asilimia 50 kwa50 ni ya kidunia, hivyo ni muhimu kuangalia jinsi ya kukabiliana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake ili kushika nafasi za uongozi na kuingia katika vyombo vya maamuzi vya kutunga sheria.

Balozi huyo, alisema midahalo ya kujadili nafasi ya wanawake na vikwazo vinavyowakabili navyo katika uongozi ni muhimu katika kuwajengea uwezo kujiandaa kuelekea Uchaguzi Mkuu utakaofanyika nchini mwaka 2025.

"Majukwaa kama haya ya kujadili masuala ya wanawake na uongozi ni muhimu hasa tunapojipanga kuelekea uchaguzi wa mwaka 2025, huku zikiwepo changamoto nyingi hasa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ambazo ni kikwazo kufikia malengo hayo," alisema Balozi Tinnes.

Alisema Serikali ya Norway itaendelea kuunga mkono juhudi za TAMWA Zanzibar kupinga vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake ili kufikia lengo la usawa wa kijinsia.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**MAKARANGA KAKULU CHARLES** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0709-0178 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia BUKONGO SEKONDARI mwaka 2021. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: PHQ/KIL/ROM/2203/2023.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA

**ARAFATI SAIDI MOHAMED** anatangaza kupotelewa na Hati ya kusafiria (Passport) yenye namba TAE387469 iliyotolewa uhamiaji makao makuu DAR ES SALAAM. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/53687/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Shauri la madai Na. 340/2023**
**Jina la Mdai ..... MJL FINANCIAL CO. LTD**
**Jina la Mdaiwa ..... NAOMI MANG'UNDA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya (18) ya Kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA: NAOMI MANG'UNDA, MAILIMBILI – DODOMA**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA TSH. 804,000/=**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 15 mwezi 12 mwaka 2023 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinanyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii Imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 11 Mwezi 12 Mwaka 2023.

HAKIMU
PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE URBAN DODOMA

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 27347 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ZEPHANIA SAASABA KYANDO**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY PETER ZEPHANIA KYANDO AND JUDITH LUBELION**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of administration is made to the above – named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 11th day of January, 2024.
DATED at KOROGWE this 11th day of December, 2023.

RESIDENT MAGISTRATE KOROGWE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No 150 of 2023**
**In the matter of the estate of the late**
**ANNA JONI RAJABU of Mpamaa within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letter of administration by DAMIANI JOHN RAJABU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN NO. 369 of 1963)**
ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20 day of 12..................... 2023
Dated at Dodoma this 20 day of 11...............2023

RESIDENT MAGISTRATE
PRINCIPAL / SENIOR / RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT COURT

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GREYSON NYANTAMBA,** Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya Toyota CRESTA, Yenye Namba za Usajili T682BMZ , Chassis Namba GX1006060754, Engine Namba 1G6565319, Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/11714/2023**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 253 LA 2023**
**CATHERINE PIUS MTEI......MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MWITA MARWA KISIBOYE......MDAIWA/WADAIWA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**MWITA MARWA KISIBOYE – POPOTE ULIPO/MLIPO**
**CATHERINE PIUS MTEI** amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 15/1/2024 saa 03:00 asubuhi/Mchana mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hii leo tarehe 07 Mwezi wa 11 Mwaka 2023.

MWENYEKITI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ISABELA ANGETILE MURAGILI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gai yenye namba za usajili T164 BUU aina ya Landrover Discovery, Chassis **No. SALLTAM231A730067**, Engine **No. 56D53059A**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ /DOD/DOD/11870/2023.**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701***

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Dunia yataka mapigano kusitishwa Gaza

**NEW YORK, Marekani**

BARAZA Kuu la Umoja wa Mataifa limepitisha azimio la usitishaji mapigano yanayoendelea Ukanda wa Gaza kati ya Jeshi la Israel na wanamgambo wa Hamas.

Upigaji wa kura hizo umekuja siku chache baada ya Marekani kutumia kura ya turufu kujaribu kuzuwia azimio hilo.

Mataifa ya Kiarabu na yenye idadi kubwa ya Waislamu yalikuwa yameitisha kikao hicho cha dharura cha baraza hilo lenye nchi 193 wanachama.

Akizungumza muda mfupi kabla ya upigaji wa kura hiyo, Balozi wa Palestina katika Umoja wa Mataifa, Riyad Mansour, alisema kuwa mataifa hayo yalikuwa yamefanya kampeni kuhamasisha uungwaji mkono wa azimio lililopitishwa.

Nchi 153 zimepiga kura ya kuunga mkono azimio hilo, wakati mataifa 10 yalipinga.

Nchi zilizopiga kura ya hapana ni Marekani, Israel, Jamhuri ya Czech, Austria, Guatemala, Liberia, Micronesia, Nauru, Papua New Guinea, na Paraguay.

Ujerumani ni miongoni mwa nchi 23 ambazo hazikupiga kura.

Katika ujumbe uliochapishwa katika mtandao wa X, Wizara ya Mambo ya Nje ya Ujerumani ilisema nchi hiyo haikuwa na chaguo lingine.

Ilisema ingawa Ujerumani inataka kumalizika kwa mateso yasiyovumilika kwa watu wa Israel na Palestina, azimio la jana lilitaka usitishaji mapigano wa jumla bila kutaja haki ya Israel kujilinda na shambulizi la kigaidi la Hamas lililofanyika Oktoba 7.

Ingawa azimio lililopitishwa halina uzito wa kisheria kama lile la awali la Baraza la Usalama, lakini linabeba ujumbe muhimu kuhusu maoni ya mataifa mengi duniani.

Azimio hilo lilionyesha kutengwa kwa Marekani na msimamo wake wa kukataa kusitisha mapigano Ukanda wa Gaza.

Marekani inachukuliwa kama upande pekee unaoweza kuishawishi Israel kusitisha mashambulizi, kwa sababu ndio mshirika wake mkuu na pia inatoa zana za kivita.

Hali halisi iliyoonekana katika kikao hicho ni mgawanyiko baina ya nchi za Magharibi na sehemu nyingine za dunia.

Pia kulishuhudiwa kuwapo kwa mpasuko wa maoni katika nchi za Ulaya. Wakati Uingereza imeungana na Ujerumani kujizuia, nchi za Ufaransa na Ugiriki zimeunga mkono azimio hilo linalotaka uwepo wa usitishwaji mapigano. Awali Rais Joe Biden wa Marekani alisema Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu anapaswa kuibadilisha serikali yake yenye msimamo mkali.

Alimwelezea kiongozi huyo kama mtu asiyetaka suluhisho la mataifa mawili linaloungwa mkono na Marekani na nchi nyingine.

Katika kile kinachoonekana kama ni ukosoaji mkali zaidi kutoka kwa Rais Biden, alisema Israel inazidi kupoteza uungwaji mkono wa kimataifa kutokana na mashambulizi yake dhidi ya Hamas Ukanda wa Gaza, ambayo yameuwa maelfu ya raia wa Kipalestina.

Wakati huo huo, kazi za upekuzi katika vituo vya mpakani vya Kerem Shalom na Nitzana umeanza ili kuongeza kiasi cha misaada inayowingia Ukanda wa Gaza.

Hata hivyo, Israel badi inaendelea na mashambulizi katika maeneo mbalimbali ya Gaza katika operesheni yao ya kuwasaka viongozi wa kundi la wanamgambo wa Hamas.

Katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika jana, Waziri wa Ulinzi wa Israel, Yoav Gallant, alikataa kuzungumzia kuhusu muda wa operesheni ya kijeshi ya nchi yake.

Gallant aliashiria kuwa awamu ya sasa ya mashambulizi ya ardhini na angani huenda ikadumu kwa wiki kadhaa zijazo au hata miezi.

Naye Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu alisema nchi yake itadhibiti usalama ndani ya ukanda wa Gaza kwa muda usiojulikana.

**DW**



Waasi wa kundi la M23 wakiendelea kuteka maeneo karibu na mji wa Goma mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo katika mapigano yanayoshika kasi. **PICHA: REUTERS**

## Kampeni za uchaguzi DRC zatawaliwa manung'uniko

**KINSHASA, DRC**

WAKATI joto la uchaguzi likizidi kupanda nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ushindani mkubwa unaendelea kuwapo kati ya Rais Filex Tshesekedi na aliyekuwa gavana wa jimbo la Katanga, Moise Katumbi.

Hata hivyo, wagombea hao wanatuhumiana kwa kila mmoja kuchochea vita mashariki mwa taifa hilo pamoja na ukabila.

Wagombea nafasi ya urais wamejikita kuweka ujumbe wa kuomba kura kutumia muziki, picha, mabango, matangazo ya redio na runinga na hata pia kwenye simu za mkononi ambao unalaumiwa kuwa na viashiria hivyo.

Uchaguzi mkuu nchini humo utafanyika Desemba 20, mwaka huu.

Tangu kuanza kampeni yake, Rais Felix Tshisekedi anayemaliza muhula wa kwanza amewanyooshea kidole mpinzani wake bila kumtaja jina akiwashutumu kwa kutumiwa na nchi za kigeni na kuunga mkono machafuko mashariki mwa nchi hiyo.

Wagombea wengine wa nafasi ya urais, Denis Mukwege na Martin Fayulu wamemshutumu Rais Tshesekedi kwa kuwazuia kufanya kampeni zao wakidai wamekosa usafiri wa ndege kwenda kuomba kura baadhi ya majimbo ya nchini humo.

Wanasiasa hao wamekilalamikia chama tawala kuwa kimenunua hazina yote ya mafuta ya ndege ili kuzuia usafiri wa ndege zitakatumiwa na wagombea wa upinzani.

Tume Huru ya Uchaguzi ya DRC (CENI) imetangaza kupokea vifaa vya mwisho vya kupigia kura kutoka nchini China kwa ajili ya upigaji kura.

**DW**

# Papa Francis ataka azikwe nje ya Vatican

**VATCAN, Roma**

PAPA Francis atakuwa kiongozi wa kwanza wa Kanisa la Katoliki duniani kuzikwa nje ya Vatican zaidi ya karne moja iliyopita.

Kiongozi huyo ambaye anatimiza umri wa miaka 87 siku ya Jumapili ijayo, alifichua mipango ya mazishi yake katika mahojiano na televisheni ya N+ ya Mexico juzi jioni.

Katika mahojiano na mwandishi wa mtandao huo wa Vatican, Valentina Alazraki, yaliyorekodiwa kabla ya Papa Francis kuongoza Ibada ya misa katika Kanisa la Mtakatifu Petro, alionekana mwenye siha njema na kupona ugonjwa wa mkamba.

Papa Francis alisema kutokana na imani yake kwa Bikira Maria, ameamua kuwa atazikwa katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Maria Maggiore lililopo mjini Roma, ambako huwa anaenda kusali kabla na baada ya kurudi safari za nje. Mapapa wengi wamezikwa chini ya jengo la Basilica ya Mtakatifu Petro.

Papa wa mwisho kuzikwa nje ya Vatican alikuwa Leo XIII, aliyefariki mwaka 1903 na kuzikwa katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Yohane wa Laterani mjini Roma.

Papa Francis alisema atakuwa tayari kujiuzulu kama mtangulizi wake Papa Benedict alivyofanya mwaka 2013, ikiwa afya yake itakuwa mbaya. Hata hivyo anaamini kuwa kujiuzulu kwa papa kusiwe jambo la kawaida.

Alipoulizwa kuhusu afya yake, alisema kwa sasa anajisikia vizuri.

Ugonjwa wa mkamba ulimlazimu Papa Francis kughairi safari ya kwenda Dubai mwezi huu kuhudhuria mkutano wa mabadiliko ya tabia nchi wa COP28.

Kiongozi huyo alifanyiwa upasuaji wa ngiri ya tumbo na alionekana kuwa amepona.

Alisema anatarajia kufanya safari tatu mwaka ujao kwenda Polynesia, Ubelgiji na nchi yake ya asili ya Argentina kwa ziara yake ya kwanza huko tangu kuchaguliwa kushika nafasi hiyo mnamo 2013.

**BBC**

HABARI MICHEZO

# JKT TANZANIA KAMILI KUIVAA KURUGENZI FA

**Na Shufaa Lyimo**

VITA ya kuwania ubingwa wa mashindano ya Kombe la FA inatarajia kuanza rasmi kwa JKT Tanzania kuwakaribisha Kurugenzi kutoka Simiyu katika mechi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Bingwa wa michuano hiyo inayofanyika kila mwaka na kudhaminiwa na Kampuni ya Azam Media hupata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Malale Hamsini, alisema baada ya kupoteza mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Azam FC hapo juzi, sasa hivi nguvu zote wameelekeza katika mchezo huo wa Kombe la FA.

Malale alisema wamejipanga kuongeza umakini na utulivu katika mechi hiyo kwa sababu wanahitaji kusonga mbele katika mashindano hayo.

Kocha huyo alisema morali ya wachezaji wake kuelekea katika mchezo huo imesharejea na wanatarajia kukutana na ushindani mkubwa.

"Maandalizi yanaendelea vyema na kila mchezaji ana morali ya juu kuhakikisha anaipa ushindi timu yetu, tutaingia uwanjani kwa tahadhari, hakuna timu ndogo, tunawaheshimu wapinzani wetu," alisema Malale.

Aliongeza tayari ameyafanyia kazi mapungufu na makosa aliyoyaona katika mchezo uliopita ili yasijirudie kwenye mechi ya leo.

Alisema wanatumia pia mchezo huo kama sehemu ya maandalizi kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union itakayochezwa Desemba 18, mwaka huu kwa sababu hawataki kupoteza pointi hata moja.

"Baada ya kumalizana na Coastal Union ya Tanga, pia tunatakiwa kujiimarisha kuwakabili Simba ambao tutacheza nao kati ya Desemba 28 na 29, mwaka huu. Mechi zote ni muhimu na tunahitaji kuvuna pointi," Malale aliongeza.

Aliwataka pia mashabiki wa timu hiyo kusahau yaliyopita na badala yake waendelee kuwapa ushirikiano ili wafanye vizuri katika michezo yote iliyobakia.




Msemaji wa Kampeni ya Magifti Dabodabo inayoendeshwa na Kampuni ya Tigo, Haji Manara (katikati) akiwa na washindi wa safari ya kwenda Dubai kwenye Uwanja wa Ndege wa Mwalimu, Julius Nyerere, Dar es Salaam muda mfupi kabla hawajaondoka nchini juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Magifti Dabodabo wapaa Dubai

**Na Mwandishi Wetu**

WASHINDI 15 walioshinda safari ya kwenda Dubai katika Kampeni ya 'Magifti dabodabo' inayoendeshwa na Kampuni ya Tigo wameondoka nchini juzi kuelekea nchini humo katika ziara ya matembezi ya siku tano, imeelezwa.

Akizungumza wakati wa kuwaaga washindi hao, Mkuu wa Huduma na Bidhaa wa Tigo, Ndevonaeli Eliakimu, alisema safari hiyo ni maalumu kwa washindi nane ambao wamechagua wapendwa wao kwa ajili kuongozana nao na kufanya idadi ya watu 16.

" Lakini watakaoondoka ni watu 15, mmoja ameshindwa kusafiri, hii ndio maana halisi ya magift dabodabo, atakayeshinda atapata nafasi ya kumchagua mpendwa wake kupewa zawadi ile ile aliyoshinda," alisema Eliakimu.

Aliongeza washindi hao wakiwa Dubai watapata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali ya vivutio huku akisema washindi wengine wataelekea Zanzibar kwa muda huo huo wa siku tano.

Bosi huyo amewataka wateja wa kampuni yao kuendelea kuchangamkia fursa ya kampeni hiyo katika kipindi hiki cha msimu wa sikukuu.

Aliwataka pia wadau kuamini kila kampeni inayotangazwa na kuwasisitiza wateja kuendelea kufanya miamala ya Tigopesa au kununua vifurushi ili kujishindia zawadi mbalimbali.

"Hii ni nafasi ya kipekee sana, sitasahau kupata fursa hii ya kutembelea Dubai na kuangalia vivutio mbalimbali, lakini kuweka rekodi ya moja ya nchi au maeneo niliyoyatembelea, nawashukuru sana Tigo kwa fursa hii," alisema Victor Munisi, mmoja wa washindi wa kampeni hiyo.

## Kitambi akaribia kujiunga Ihefu SC

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Namungo umeweka wazi umeachana rasmi na aliyekuwa Kaimu Kocha Mkuu, Denis Kitambi na timu hiyo itakuwa chini ya mwalimu wa viungo, Shadrak Nsajigwa na Mrundi, Vladimir Niyokuru.

Taarifa zilizopatikana jijini zinasema Kitambi anatajwa kuwa katika mazungumzo na Ihefu ambayo hivi karibuni ilitangaza kuachana na aliyekuwa Kocha Mkuu, Moses Basena.

Ofisa Habari wa Namungo, Kindamba Namlia, alisema wameachana na kocha huyo baada ya kufikia makubaliano ya pande mbili, lakini wanamshukuru kwa muda wote aliokuwa katika kikosi chao kinachoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunamtakia kila la kheri Kocha Denis Kitambi katika safari yake ya ukocha nje ya Namungo," alisema Namlia.

Imeelezwa awali, Ihefu ilikuwa inamhitaji Juma Mgunda, lakini imeshindikana kutokana na kocha huyo kuwa na mkataba na Simba akiwa na cheo cha Mkurugenzi wa Ufundi, akihudumu hasa katika timu za vijana na Simba Queens.

## Mlandege: Tutatetea Kombe la Mapinduzi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Msaidizi wa Mlandege, Jaala Abdallah, amesema malengo ya timu hiyo ni kupambana na kuhakikisha wanatetea ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambalo wanalishikilia.

Mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yatafanyika kuanzia Desemba 28 hadi Januari 13, mwakani yanatarajiwa kushirikisha timu 12 kutoka sehemu mbalimbali.

Abdallah alisema dhamira na ari yao kuelekea mashindano hayo ni kubwa na wanaahidi kuwapa furaha Wazanzibar kwa kulibakisha kombe hilo nyumbani.

"Tumedhamiria kufanya kama tulivyofanya mwaka huu kuchukua ubingwa, tayari tumeshafanya kikao na benchi la ufundi pamoja na wachezaji kwa ajili ya kuongeza hamasa ili wawe katika nyakati nzuri katika michuano hii," alisema kocha huyo.

Timu zitakazochuana kuwania ubingwa wa mashindano hayo ni Mlandege FC, Jamhuri , Chipukizi na KVZ, Simba, Yanga, Azam FC, Singida Fountain Gate, APR (Rwanda), URA (Uganda), Bandari (Kenya) na Vital'O FC ya Burundi.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**DE BEEK KUTUA FRANKFURT**

MAZUNGUMZO yatakayomwezesha kiungo wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Donny van de Beek, mwenye umri wa miaka 26 kujiunga na Eintracht Frankfurt kwa mkopo yamepiga hatua. **(Fabrizio Romano)**

**CELSO ANUKIA SPURS**

BARCELONA inatazamia kumnunua kwa mkopo kiungo wa Tottenham Hotspur na Timu ya Taifa ya Argentina, Giovani Lo Celso, mwenye umri wa miaka 27 katika dirisha la uhamisho litakapofunguliwa Januari. **(90min)**

**MOURINHO ATAJWA NEWCASTLE**

WAMILIKI wa Newcastle United wanavutiwa na Jose Mourinho, huku mkataba wa kocha huyo wa AS Roma mwenye umri wa miaka 60 ukitarajiwa kumalizika msimu ujao baada ya tetesi kuibuka klabu hiyo ya Serie A haina nia ya kubaki na Mreno huyo. **(Gazzetta dello Sport)**

**GREENWOOD KUBAKI GETAFE**

KLABU ya Getafe inamatumaini ya kumnunua mshambuliaji wa England, Mason Greenwood, mwenye umri wa miaka 22 kutoka Manchester United na watafaidika kutokana na kipengele cha mauzo cha asilimia 20 ambacho kiliwekwa katika mkataba wake wa mkopo kwa klabu hiyo ya LaLiga. **(Athletic)**

**LEONARDO KUTUA ARSENAL**

KLABU ya Arsenal imetoa ofa ya pauni milioni 17.2 pamoja na nyongeza kwa mshambuliaji wa Santos na Timu ya Taifa ya umri chini ya miaka 20 ya Brazil, Marcos Leonardo. **(Fichajes)**

**CITY YAHITAJI STRAIKA**

KLABU ya Manchester City inaweza kumnunua kiungo na mshambuliaji mpya katika dirisha la uhamisho la wachezaji litakapofunguliwa Januari. **(Football Insider)**

**PHILLIPS KUSAJILIWA JUVE**

JUVENTUS bado imeonyesha nia ya kumsajili kwa mkopo kiungo wa Manchester City na Timu ya Taifa ya England, Kalvin Phillips, mwenye umri wa miaka 28 ifikapo Januari. **(Gazzetta dello Sport)**

**CHELSEA YAMTAKA GYOKERES**

CHELSEA inamtaka mshambuliaji wa Sporting Lisbon na Timu ya Taifa ya Sweden, Viktor Gyokeres, mwenye umri wa miaka 25. **(Ekrem Konur on X)**

**LOPETEQUI ANUKIA PALACE**

KOCHA wa zamani wa Wolves na Hispania, Julen Lopetegui, mwenye umri wa miaka 57 anawaniwa na klabu za Crystal Palace na Nottingham Forest. Mhispania huyo hajafanikiwa kupata kazi tangu Agosti, mwaka huu alipoondoka Wolves. **(Sun)**

**KONATE, LIVERPOOL KITAELEWEKA**

MLINZI wa Liverpool, Ibrahima Konate, mwenye umri wa miaka 24 ameanza mazungumzo ya kuongeza mkataba mpya na Wekundu hao, licha ya uvumi unaomhusisha anajiandaa kuhamia Paris St-Germain. **(le10sport)**

**GUIRASSY AGOMBEWA ULAYA**

KLABU ya Borussia Dortmund imejiunga na Newcastle United katika kinyang'anyiro cha kuwania saini ya Serhou Guirassy, mshambuliaji wa Stuttgart na Guinea, mwenye umri wa miaka 27. Guirassy tayari amefunga mabao 16 katika Ligi Kuu Ujerumani msimu huu. **(Bild Sports)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG : SASA MACHO YOTE EPL

Kocha huyo asema bado kikosi chake kinatakiwa kupambana ili...

**MANCHESTER, England**

KOCHA Erik ten Hag amekiri Manchester United "ilipaswa kufanya vyema zaidi" katika Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, lakini akasema kuondolewa kwao mapema hakumaanishi msimu wao umefikia mwisho.

Kipigo cha United cha 1-0 kutoka kwa Bayern Munich, pamoja na ushindi wa 1-0 wa FC Copenhagen dhidi ya Galatasaray, kiliifanya timu hiyo ya Ten Hag kuondolewa kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kumaliza mkiani katika Kundi A.

Mholanzi huyo alisema baadaye timu yake bado ina mambo mengi ya kufanya, licha ya kutolewa kwenye Kombe la Carabao na kushika nafasi ya sita katika msimamo wa Ligi Kuu England.

"Ukweli ulioko hatuna pointi za kutosha," alisema Ten Hag.

"Tumesikitishwa kama kundi, kama kocha nimesikitishwa, tulipaswa kufanya vizuri zaidi. Bado kuna mechi nyingi za kucheza na sasa tunaweza kuzingatia, bila shaka, kwenye Ligi Kuu.

"Hiki ndicho kiwango tunachotaka kucheza Ligi ya Mabingwa, hivyo tunatakiwa kujituma ili tuwe katika nafasi nne za juu na mwakani turudi kwenye Ligi ya Mabingwa, halafu tuna Kombe la FA, kwa hiyo bado kuna mambo mengi."

Lilikuwa ni jaribio la kupata matokeo chanya kutoka kwa Ten Hag, lakini kushindwa kwa mara ya 12 msimu huu, mechi saba kati yao wakiwa nyumbani -- ni pigo lingine kubwa.

Ili kufanya mambo kuwa mabaya zaidi, Harry Maguire na Luke Shaw walipata majeraha ya misuli dhidi ya Bayern Munich na sasa wanaweza kukosa safari ya Anfield kucheza dhidi ya vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool hapo Jumapili.

"Tunapoteza wachezaji ambao wana maamuzi makubwa kwa mchezo wetu, ambao wanaweza kuleta mabadiliko na katika michezo mingi ndivyo ilivyokuwa katika kampeni hii," alisema Ten Hag.

"Si mara zote hatukuwa na wachezaji tunaotaka kucheza. Hiyo ni sehemu muhimu.

"Sasa nakupa sababu, lakini usione kama kisingizio kwa sababu hata wakati hatuko wote kwenye kundi, bado tunapaswa kushinda kwa sababu Manchester United ni kundi kubwa."

## HABARI MICHEZO



# BENZEMA, KANTÉ WAIBEBA AL ITTIHAD KLABU BINGWA

**RIYADH, Saudi Arabia**

MABAO ya kipindi cha kwanza kutoka kwa Romarinho, N'Golo Kanté na Karim Benzema yaliiwezesha Al Ittihad kupata ushindi wa magoli 3-0 dhidi ya Auckland City na kutinga raundi ya pili ya michuano ya Kombe la Klabu Bingwa ya Dunia katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa King Abdullah Sports City hapo juzi.

Wakicheza kwa mara ya kwanza katika michuano hiyo tangu walipotinga nusu fainali mwaka 2005, Al Ittihad walitawala mchezo huo wa nyumbani na sasa kesho watacheza dhidi ya mabingwa wa Afrika, Al Ahly kwenye uwanja huo huo.

Mshindi wa mchezo huo atacheza na mabingwa wa Copa Libertadores (Ligi ya Mabingwa wa Amerika Kusini), Fluminense katika hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo.

Wenyeji walianza kupata bao kupitia kwa Romarinho aliyefunga kwa shuti kali kutoka pembeni ya eneo la goli na kumshinda mlinzi wa timu pinzani na kutinga wavuni mpira ukimpita golikipa, Conor Tracey.

Kiungo wa kati wa Ufaransa, Kanté alifunga bao la pili dakika tano baadaye kwa shuti kutokana mpira uliozagaa ndani ya eneo la hatari kabla ya mwenzake Benzema kuongeza goli la tatu dakika ya 40 na kuwa mchezaji wa kwanza kufunga katika michuano minne tofauti ya Kombe la Klabu Bingwa ya Dunia.

Washindi wa Ligi ya Mabingwa wa Concacaf, Leon, watamenyana na mabingwa wa Asia, Urawa Red Diamonds katika mechi yao ya raundi ya pili hapo kesho.

Mshindi katika mechi hiyo atakutana na mabingwa wa Ligi Kuu England, Manchester City.

# Klopp afurahia kumkosa Caicedo

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amedokeza Liverpool walikuwa na "bahati" kukosa kumsajili, Moises Caicedo, ambaye hakuwa na kiwango bora katika msimu uliopita na badala yake wakamalizana na Wataru Endo.

Liverpool walikuwa wameingia katika mvutano wa muda mrefu wa uhamisho na Chelsea kuhusu Caicedo wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto, huku kiungo huyo akijiunga na The Blues kwa ada ya milioni 115 ambayo iliweka rekodi England.

Wekundu hao walikubali kwanza ada ya pauni milioni 111 kabla ya Chelsea kuongeza ofa yao.

Akizungumza katika hafla ya majaribio kwa jukwaa jipya lililorekebishwa pale Anfield Road, Klopp alijadili sakata hilo na akakiri anahisi Liverpool walikuwa na "bahati" kukosa walengwa wao wakuu.

"Majira ya joto tulikuwa na mambo machache ya ajabu kutokea katika soko la uhamisho lakini hapa, kati yetu, naweza kusema, 'Mungu wangu, tulikuwa na bahati,'" alisema Klopp.

"Ni wazi tuligundua viungo wengine wa kati wa safu ya ulinzi hawataki kujiunga na Liverpool, unaona kinachotokea, na ndipo tukampata (Wataru), Endo. Ni mchezaji wa kipekee."

Ingawa Liverpool walimkosa Caicedo, Wekundu hao walifanikiwa kusajili viungo wanne wa kati wakati wa usajili wa majira ya joto.

Kikosi cha Klopp kilitumia takribani pauni milioni 150 kuboresha safu yao ya kiungo kwa kuwanasa Dominik Szoboszlai, Alexis Mac Allister, Ryan Gravenberch na Endo, ambaye alisajiliwa mara baada ya Caicedo kwenda Chelsea.

Ingawa safu hii mpya ya kiungo imeisaidia Liverpool kupaa kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu England, safu ya kiungo ya Chelsea inayoongozwa na Caicedo imekuwa na matatizo makubwa katika kipindi cha kwanza cha msimu wa 2023/24.

Kiungo huyo wa zamani wa Brighton amejikuta akiingia na kutoka katika kikosi cha kwanza cha Kocha, Mauricio Pochettino kutokana na uchezaji wake usiobadilika kwa Chelsea ambayo haikufanya vizuri.

The Blues wamejikuta katika nafasi ya 12 kwenye msimamo, wakiwa wamepoteza michezo saba tayari msimu huu.

# James kurejea dimbani Februari

**LONDON, England**

NAHODHA wa Chelsea, Reece James, anatazamiwa kuonana na mtaalamu wa misuli ya paja katika jitihada za kufahamu tatizo lake la hivi karibuni, lakini kuna uwezekano mkubwa akawa nje ya dimba hadi Februari, mwakani.

James ana historia ya matatizo ya misuli ya paja na alitolewa uwanjani wakati wa kipindi cha kwanza katika mechi ya Ligi Kuu England ambayo Chelsea walichapwa na Everton iliyochezwa Jumamosi iliyopita.

Tayari msimu huu, hajacheza kwa miezi miwili kutokana na tatizo sawa na hilo wakati wa mechi ya ufunguzi hapo Agosti, mwaka huu.

Inaripotiwa James anatarajiwa kukosa kucheza soka kwa takribani miezi mitatu na hataweza kurejea hadi mwisho wa Februari au mwanzoni mwa Machi.

James mwenye umri wa miaka 24 anakutana na mtaalamu wa misuli ambapo itajumuisha uchunguzi ili kuelewa undani wa tatizo.

Akiwa pia na matatizo mbalimbali ya kifundo cha mguu na goti katika miaka ya hivi karibuni, James anakadiriwa kukosa mechi 35, karibu na msimu mmoja kamili wa Ligi Kuu, kutokana na majeraha ya nyama ya paja pekee.

Kocha Mkuu wa Chelsea, Mauricio Pochettino, alichukizwa na kushindwa kwa hivi punde zaidi kutokana na athari ya kumpoteza mchezaji huyo muhimu na mwenye ushawishi wakati ambapo The Blues wako katika mradi mkubwa wa kujenga timu.

"Bila shaka kwetu sisi ni mchezaji muhimu, mmoja wa mabeki bora zaidi duniani," alisema Pochettino.

"Tumesikitishwa kwa sababu unapoamini unaweza kujenga kitu na mchezaji kama yeye ambaye anafaa kuwa muhimu kwetu hawezi kuisaidia timu."

Kwa bahati mbaya kwa Chelsea, mlinzi wa pili wa kulia Malo Gusto anaendelea kukosekana pia.



## HABARI MICHEZO

# MGUNDA ATAMBA KUREJESHA HESHIMA YA SIMBA QUEENS

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Juma Mgunda, amesema kutwaa ubingwa wa kwanza wa Ngao ya Jamii ni ishara nzuri kwao kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania inayotarajiwa kufanyika kuanzia Desemba 20, mwaka huu.

Simba Queens imetwaa ubingwa huo baada ya kuifunga JKT Queens penalti 5-4 kufuatia sare ya bao 1-1, katika dakika 90 za kawaida.

Stumai Abdallah alifunga bao kwa upande wa JKT Queens dakika ya 20 huku Danai Bhobho aliisawazishia Simba Queens dakika saba baadaye.

Akizungumza na Nipashe jana, Mgunda, alisema kutwaa Ngao ya Jamii imempa mwanga wa kufahamu mapungufu ya kikosi chake na atayafanyia kazi kabla ya kuanza kwa msimu mpya siku chache zilizobakia.

Mgunda alisema mechi ya fainali ilikuwa na ushindani mkubwa kutokana na wapinzani wao walikuwa bora ndani ya dakika 90, lakini pia wachezaji wake walipambana kuhakikisha wanafikia katika malengo yao.

"Haikuwa mechi rahisi, fainali ilikuwa ya ushindani na mchezo mgumu kwa timu zote, kwetu na wapinzani wetu JKT Queens, tumeona wachezaji wamepambana ili kusawazisha bao na kwenda hadi kwenye matuta.

Niwapongeze sana wachezaji wangu kwa kufuata yale niliyowaelekeza, fainali hii kwetu ni ishara nzuri kwa kuona mwanga mzuri tunapoelekea katika mechi zetu za Ligi Kuu," alisema Mgunda.

Kocha huyo amewataka mashabiki wa Simba kuwa na subira pale wanapoona timu 'inateleza' kwa sababu mpira wa miguu una matokeo katili.

Kiungo Mkabaji wa Simba Queens, Vivian Corazone, alitangaza kuwa Mchezaji Bora wa mashindano hayo huku tuzo ya Kipa Bora ikichukuliwa na kipa wa mabingwa hao, Carolyene Rufa wakati Stumai akibeba tuzo mbili, Mchezaji Bora wa mechi ya fainali na Mfungaji Bora wa michuano hiyo ya kwanza kufanyika.




Mabingwa wa kwanza wa Ngao ya Jamii kwa Wanawake Tanzania, Simba Queens wakifurahia baada ya kuibuka washindi katika mechi ya fainali ya michuano hiyo iliyochezwa juzi jioni. Simba Queens iliwafunga JKT Queens kwa penalti 5-4. **PICHA: TFF**

# Bajana avunja rekodi bao la mapema Bara

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Azam, Sospeter Bajana, amevunja rekodi ya bao la mapema katika Ligi Kuu Tanzania Bara iliyokuwa inashikiliwa na mchezaji wa Dodoma Jiji, Yassin Mgaza.

Kwa mujibu wa takwimu zetu na za Bodi ya Ligi zilizotolewa jana, Bajana alifunga bao sekunde ya 54, Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Azam Complex, katika mechi dhidi ya JKT Tanzania, timu yake ikiondoka na ushindi wa mabao 2-1.

Kwa sasa Bajana ndiye anayeshikilia rekodi ya bao la mapema zaidi katika ligi hiyo akivunja rekodi ya Mgaza ambaye alifunga dakika ya pili ya mchezo katika mechi dhidi ya Tabora United iliyochezwa Oktoba 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora.

Awesu Awesu wa KMC na Zidane Sereli wa Dodoma Jiji wakishika nafasi ya pili kwa kufunga bao dakika ya pili kila mmoja.

Feisal Salum wa Azam, Pacome Zouzua na Kennedy Musonda kutoka kwa mabingwa watetezi, Yanga wanafuatia kwa mabao ya mapema, ambapo kila mmoja alifunga bao dakika ya tatu ya mchezo kwenye mechi tofauti ambazo timu zao zimecheza.

## Bonito, Mutale wakaribia Yanga

INATOKA UK. 24

chuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara, kuna Kombe la FA ambalo halijaanza na Kombe la Mapinduzi.

Tunataka ikifika mzunguko wa pili, hawa tunaowaongeza wawe wameshapatikana, dirisha likifunguliwa kazi yetu itakuwa ni kutangaza wachezaji na si kutafuta, tumeshazungumza na nyota tunaowahitaji ili dirisha dogo likifika wanajiunga haraka na kikosi kwa sababu hakuna muda wa kusubiri," Kamwe alisema.

Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limesema tayari FIFA imeifungulia Yanga kifungo chake baada ya kukamilisha malipo ya aliyekuwa mchezaji wake, Gael Bigirimana, ambaye alikuwa akiidai klabu hiyo.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema jana mchezaji huyo alifungua kesi FIFA dhidi ya Yanga kwa kushindwa kumlipa madai yake baada ya kuvunja mkataba.

Ndimbo alisema Bigirimana alishinda kesi hiyo na Yanga ilitakiwa kumlipa ndani ya siku 45 tangu uamuzi huo ulipotolewa, lakini haukutekelezwa na kusababisha kupata adhabu ya kuifungia.

Wakati huo huo, Yanga tayari imekamilisha usajili wa kiungo wa JKU FC na Timu ya Taifa ya vijana Zanzibar, Shekhan Ibrahim, kwa kumpa mkataba wa miaka mitatu.

Katibu Mkuu wa JKU, Shadhily Khatib, alisema nyota huyo kwa sasa sio mali yao baada ya kukamilisha taratibu za kujiunga na Yanga na kinachosubiriwa ni dirisha dogo la usajili kufunguliwa rasmi.

"Ni kweli kwa sasa Shekhan sio mchezaji wetu kwa sababu amesaini mkataba wa miaka mitatu na tumeshamalizana na Yanga, " alisema Katibu huyo.

## Mfalme Shangwe kuibeba Simba SC

INATOKA UK. 24

da, kwa sababu eneo kubwa ambalo litafaidika kwa kampeni hii ni kuendeleza soka la vijana U-17," alisema Kajula.

Aliongeza Simba inapozungumzia ndoto za kuchukua ubingwa wa Afrika, unatakiwa kutengeneza misingi imara ya soka la vijana ambao hapo baadaye watakuwa msaada wa klabu na timu za taifa.

"Ushiriki wa shindano kama hili sio kufaidisha klabu, lakini shabiki anachangia klabu yake uwezo wa kifedha pamoja na kutoa mchango wa kimawazo juu ya usajili na mambo mengine katika kuhakikisha klabu inasonga mbele," Kajula aliongeza.

Alisema pia matarajio ya Simba ni kuona mashabiki wanakuwa karibu na timu yao na viongozi watambua mchango huo na kuhakikisha wanaendelea kuwapa furaha mashabiki wao katika kufanya vizuri kwenye michezo mbalimbali ikiwamo kufikia malengo ya kutinga hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

# Michezo

Alhamisi Desemba 14, 2023

Nipashe




## Ten Hag : Sasa macho yote EPL

UKURASA 21

# BONITO, MUTALE WANUKIA YANGA SC

●●●Yamnasa rasmi Shekhan wa JKU, yatamba usajili wao utatikisa...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), likiwaondolea kifungo cha kufanya usajili, Yanga imepanga kusajili wachezaji nyota wapya ili kukiongozea nguvu kikosi chao kinachohitaji kufanya vizuri katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Habari zilizopatikana kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema mbali na straika, Ranga Chivaviro, kutoka Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara wameanza mazungumzo ya kuwasajili, Benson Mangolo wa Jwaneng Galaxy ya Botswana na Bonaventure Bonito wa Tengueth ya Senegal.

Chanzo hicho kilisema winga wa Power Dynamo ya Zambia, Joshua Mutale, naye yuko katika rada za Yanga pamoja na mshambuliaji wa Medeama, Jonathan Sowah na Daniel Adjetey, wote raia wa Ghana.

Hata hivyo, Yanga itapambana na watani zao Simba katika kuwania saini za Mangolo na Mutale huku nyota Adjetey akitajwa kutakiwa na Geita Gold FC ya mkoani Geita.

Chanzo hicho kiliongeza Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amemtaja Bonito kuwa ndiye mchezaji namba moja anayemhitaji katika kikosi chake kwa ajili ya kumsaidia, Khalid Aucho, ambaye akikosekana ama kwa kutumikia adhabu ya nje au majeruhi, anakosa mbadala sahihi.

"Tangu aondoke Mayele (Fiston), tunahaha upande wa straika, Hafiz Konkoni siyo mchezaji mbaya, ila ni kwa sababu aliyeondoka alikuwa na kiwango cha hali ya juu na hiki ndicho kitakachowahukumu mastraika wote watakaotua hapa.

Wanachama na mashabiki wanatataka kuwalinganisha na Mayele. Huenda Sowah wa Medeama na Chivaviro wanaweza kujaribu kuvaa viatu vya Mayele," kilisema chanzo chetu.



Mutale

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, aliiambia gazeti hili tayari Gamondi ameshawasilisha ripoti yake ya ufundi muda mrefu na imeshaanza kufanyiwa kazi.

Kamwe alisema Yanga imedhamiria kufanya vizuri zaidi katika msimu huu na ili ifikie malengo yake, inatakia kuimarisha kikosi chake kwa kusajili wachezaji wenye ubora na uzoefu wa kucheza mashindano ya kimataifa.


"Gamondi ameweka wazi ni maeneo gani yanatakiwa kufanyiwa marekebisho, ni aina gani ya wachezaji wanaotakiwa kuja kuiongezea nguvu timu katika mi-

INAENDELEA UK. 23

## JKT Tanzania kamili kuivaa Kurugenzi FA

VITA ya kuwania ubingwa wa mashindano ya Kombe la FA inatarajia kuanza rasmi kwa JKT Tanzania kuwakaribisha Kurugenzi kutoka Simiyu katika mechi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

HABARI UK. 20



## Benzema, Kanté waibeba Al Ittihad Klabu Bingwa

MABAO ya kipindi cha kwanza kutoka kwa Romarinho, N'Golo Kanté na Karim Benzema yaliiwezesha....

HABARI UK. 22



## Mgunda atamba kurejesha heshima ya Simba Queens

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Juma Mgunda, amesema kutwaa ubingwa wa kwanza wa Ngao ya Jamii ni ishara...

HABARI UK. 23



Imani Kajula

# Mfalme Shangwe kuibeba Simba SC

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inakiongeza nguvu kikosi chake ili kufanya vizuri kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa Simba umetangaza kuzindua kampeni mpya ya kuwasogeza karibu mashabiki wake iitwayo 'Mfalme Shangwe', imefahamika.

Mshindi wa shindano hilo atapata fedha na tiketi za kuingia uwanjani katika mechi za nyumbani na ugenini.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema wanatambua mchango wa mashabiki wa klabu hiyo kwa kununua bidhaa au kuhudumia klabu yao kwa lengo la kusaidia uendeshaji.

Kajula alisema ili kuendesha klabu vizuri zinatakiwa fedha na kwa sasa bajeti ya mwaka ya klabu yao ni zaidi ya bilioni 20 na anaamini kampeni waliyoizindua itasaidia kufikia malengo.

Alisema kampeni hiyo itatoa mchango mkubwa katika uendeshaji wa klabu kupitia mashabiki.

"Tunatambua mchango wao na sasa tumekuja na shindano hilo ambalo litakuwa na fedha taslimu Sh. milioni 500 na tiketi za kushuhudia michezo ya timu yao nyumbani na ugenini.

Mashabiki na wadau wa Simba kwetu wanafai-

INAENDELEA UK. 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >